

UIGAJI WA UKRISTO



Asante. Asante, Ndugu Vayle. Daima inajulikana kwamba ni majaliwa kuketi katika mahali pa Kimbinguni katika Kristo Yesu pamoja na watu Wake. Na leo nilipata majaliwa makuu ya kutembelea kanisa la Ndugu yetu mchungaji, ndipo tukawa na wakati mzuri wa ushirika pamoja, tulipokuwa tumeketi katika mahali pa Kimbinguni kwenye kanisa la Kibaptisti asubuhi ya leo.

² Halafu pamoja na cha—chakula cha mchana pamoja na Dk. Wierwille (kamwe siwezi kulitamka hilo vizuri.), na ndugu zake, na wengine zaidi, da—daktari, daktari wa meno, na kikundi fulani ambacho tulikula chakula cha mchana pamoja nao muda mfupi uliopita. Na hii bila shaka imekuwa siku ya furaha, nami nikitumaini kwa Mungu kwamba itaendelea kuwa hivyo siku nzima kwa ajili yetu sote, kwa kuwa tumekutana pamoja tena katika Kristo, kuketi tu katika mahali pa Kimbinguni pamoja Naye.

³ Basi nimepata majaliwa ya ku—kuzungumza nanyi tena alasiri ya leo. Kidogo nimepwelewa na sauti, kwa sababu ya, vema, nilikuwa na mafua kidogo tu nikija, nami... Kidogo inalemea damu yetu ya kusini, mnajua. Kidogo ni baridi huku juu na ni baridi kidogo kuliko ilivyo nyumbani; halafu kusafiri huku na huku sana.

⁴ Juma moja, sasa, juma... Katika yapata juma lingine moja au siku kumi, Bwana akipenda, nitakuwa Phoenix, Arizona, ambako watoto wote ni miguu tupu, wakikimbia huku na huku, kisha kuelekea California, halafu kupanda Pwani ya Magharibi tena ambako kunaganda tena. Na hivyo ndivyo ibada za uinjilisti zinavyokwenda, ama, maisha yanavyokwenda, hasa, kwa mwinjilisti. Lakini ni majaliwa makubwa sana kumtumikia Bwana. Jinsi nilivyo na furaha.

⁵ Pia ni, inaonekana kana kwamba mtu angesema, “Ndugu Branham, nadhani maisha yako yote ni maisha ya ushindi.” Loo, ni kwamba tu hujui yote. Loo, ni—ni maisha ya ushindi, kama mnavyoyajua kuwa katika Kristo. Loo, ni majaliwa jinsi gani kwangu kujua ya kwamba Yeye huniruhusu kuzungumza na watoto Wake na jinsi ambavyo tunakusanyika pamoja na kuongea, kuzungumza, na kuabudu. Hilo ni zuri sana. Lakini kuna mambo yanayoambatana nayo; ni vigumu sana, kama vile kuiacha familia kwa kuanzia. Nina familia nzuri na mvulana mdogo ambaye wakati...

⁶ Nimefunga ndoa mara mbili. Mke wangu wa kwanza alikufa wakati... maskini msichana wangu mdogo alikuwa na umri wa miezi minane tu, naye mtoto Billy alikuwa na umri wa

miezi kumi na minane tu. Mke alikuwa na umri wa miaka ishirini na miwili, nafikiri, nami nilikuwa na karibu ishirini na sita. Na mimi—mimi nikampoteza, naye. . . Sa—sa—samahani sikukusudia kusema hilo hivyo. Kamwe sikumpoteza. Yeye alipanda tu kwenda juu, na. . . yeye pamoja na huyo mtoto mchanga. Nami nilikuwa na Billy kwa miaka mingi, halafu alipoenda shuleni, Bwana akanipa maskini mke mzuri, nasi tulikuwa tumefunga ndoa kwa muda wa miaka minne ndipo msichana mdogo, Rebekah, akaja.

⁷ Miaka mingine minne, kwenye wakati huo, nilikuwa Minneapolis wakati mmoja mkutanoni, ambapo ninaenda kwa mkutano wangu unaofuata; baada ya hapa ninaenda Evansville halafu Minneapolis, kisha Phoenix, baada ya kusimama kidogo huko Louisiana. Kwa hiyo basi, nilikuwa kule juu, nami nilikuwa nikiyachukua maisha ya Yusufu, nikisoma tu maisha yake. Nanyi mwajua, Ibrahimu, ilivyohubiriwa asubuhi ya leo, Ibrahimu alikuwa ni uteuzi. Ndipo Ibrahimu akamzaa Isaka, ambaye ni kuhesabiwa haki. Isaka akamzaa Yakobo, ambaye ni neema. Kisha Yakobo akamzaa Yusufu, ambaye ni ukamilifu, hamna jambo moja dhidi ya Yusufu. Nami nikayaona maisha yake makuu, ndipo nikasema, “Ee Mungu, kama. . .”

⁸ Na mimi—mimi kwa namna fulani ni mtu mwenye akili ndogo, kama mnavyojua tayari. Basi nikaingia katika chumba kidogo, kwa sababu, vema, naye Mungu atayasikia maombi yako popote pale, lakini alisema, “Ingia kwenye chumba cha siri,” pia. Na loo, nadhani kuna ya kutosha tu kunihusu mimi kwamba sijakua vizuri bado katika miaka hii yote arobaini na saba, kwa hiyo niliingia tu chumbani na kufunga mlango. Nami nilikuwa tu nikilia kwa furaha.

⁹ “Loo,” nikasema, “nitafurahi sana siku moja nitakapovuka huko kukutana na Yusufu na kumpa mkono; nimwone Danieli na kumwuliza jinsi alivyojisikia wakati wale simba walipomkimbilia, nayo Nguzo ile ya Moto wa Nuru ikasimama pale na kuwazuia hao simba usiku kucha; niwaone wale wana wa Kiebrania, jinsi walivyotoka kwenye ile tanuru ya moto huku upepo wa Kipentekoste ukiwazunguka, ukizunguka-zunguka, ukiuzuia upepo mwanana.” Nikasema, “Ni wakati mzuri jinsi gani.” Ndipo nikasema, “Ee, Mungu, kama ukiwahi kunipa mtoto, nitamwita jina lake Joseph (mvulana).” Naye Billy alikuwa mvulana mkubwa kidogo wakati huo. Na halafu, mnajua, nilipoangalia, nikaingia kwenye, vema, sijui niliiteje, siwezi kuelezea hilo, sitaki. . . Ni: huwezi kumwelezea Mungu; Mungu haelezeki.

¹⁰ Ikiwa kungekuwa na mtu hapa ambaye angependa kulikaribia katika kile ninachoita “milki ya kisayansi”: Juu katika kiwango kingine, uko mahali pengine, ni halisi tu kama hapa palivyo, lakini uko tu mahali pengine, na unajua uko pale, lakini unajua sauti yako iko hapa, lakini uko pale. Unaona?

Ati nipaeleezee? Siwezi. Lakini kitu Fulani kilisema, “Utapata mwana, nawe utamwita jina lake Joseph.”

Loo jamani, moja kwa moja kutoka kwenye huo mkutano, “Nitapata mvulana jina lake Joseph.”

¹¹ Vema, baada ya kitambo kidogo tulijua kwamba tutampata mtoto. Kila mtu akasema... Naye mke wangu, watu wake na wote hao inabidi wazae kwa upasuaji. Na kwa hiyo daktari akasema, baada ya Rebekah kuzaliwa, alisema, “Huyo anapaswa kuwa wa mwisho, kwa sababu ya hali fulani, kwamba kamwe hapaswi kuzaa watoto tena.”

“Vema,” nikasema, “Bwana mwema anajua yote kuhusu hayo.”

Na—na kwa hivyo basi tu—tulijua tutampata mtoto mchanga, kwa hivyo tukashangaa kama... Baadhi yao wakasema, “Huyo ni Joseph?”

Nikasema, “Sijui,” nikasema, “lakini tutampata Joseph, kwa hiyo,” nikasema, “kwa namna fulani ninaamini ndiye.”

Basi alipozaliwa, alikuwa ni msichana. Loo, nena kuhusu kunishambulia vikali. Kila mahali, nilipata barua, zilizosema, “Nilidhani ati maono yako hayakudanganya.”

“Hayadanganyi kamwe.” Nikasema, “Joseph anakuja.”

¹² Na kwa hiyo daktari alipomleta maskini huyo msichana mdogo, alisema, “Loo, Bw. Branham,” alisema, “mwembamba kwelikweli,” kasema, “tunapaswa kufanya kitu kuhusu hili,” akasema, “kwamba wao...hakuna watoto zaidi wanguweza kuja.”

Nikasema, “Loo, la, Joseph yuaja.” Na kwa hiyo, tukisimama pale...

Ndipo baada ya kitambo kidogo, wakati, ukaendelea, miaka minne ikapita. Baadhi yao wakaendelea kusema, “Vema, huo ni wakati mmoja lilishindwa.”

Nikasema, “La. Mnakumbuka, kamwe sikusema huyo alikuwa Joseph. Nilisema, ‘Joseph anakuja.’”

¹³ Kwa hivyo baada ya kitambo kidogo tulijua tutampata mtoto mwingine, baada ya miaka minne zaidi, tulikuwa tunaenda kumpata mtoto mwingine. Vema, nikasema, “Vema, natumaini huyu ni Joseph.”

Kwa hiyo basi baada ya kitambo kidogo, mbona wao, hao wote, wakasema, “Je, huyu ni Joseph?”

Nikasema, “Sijui mimi. Lakini Joseph anakuja.”

¹⁴ Kwa hiyo tuliposhuka moja kwa moja, siku chache tu, kwa uzazi wa Kupasuliwa, na, vema, mambo ambayo nisingeweza kunena mbele ya kusanyiko lililochanganyikana, bali wanapaswa kuingia, kwenye, kwa ajili ya upasuaji wao, mapema sana kabla ya wakati. Na kulikuwako na mama

fulani anayeishi humo mjini, kwamba maskini mama huyo alichanganyikiwa kabisa, hata alifikiria kwamba anapaswa kuwa kiongozi wa kiroho wa maisha yangu, na aniambie niende wapi, na nifanye nini. Niliyakataa tu hayo, kabisa, mnaona, kwa sababu, Roho Mtakatifu hufanya hayo.

¹⁵ Na kwa hiyo, alikuwa akisambaza kadi, ndipo akasema, “Sasa, hapa ndipo Billy *atakapojitia*,” kasema, “Mungu atamwondoa Meda kwake sasa.” Naye akayaandika yote na kuyaeneza nchini kote, mwajua. Basi mke wangu, akiwa mwenye wasiwasi kwa vyovyote vile, loo, maskini jamaa huyo alikuwa karibu kufa.

Naye akaja, akasema, “Loo, Bill, ulisikia hilo?”

Nami nikasema, “Loo, hilo halileti tofauti yoyote. Mungu alisema tutampata huyo mtoto, na hilo latosha.” Kwa hiyo sisi . . .

¹⁶ Basi ikanibidi kuwazia, mnajua, naye akiwa amedhoofika sana, nilienda tu mahali fulani; nina mahali pa siri (Mmesikia habari zake.), huko nyuma kabisa ninakoingia pangoni, na kurudi nyuma; FBI isingeweza kunipata. Kwa hiyo ni—nikarudi mle ndani. Nilikuwa huko nyuma nikiomba, naye Bwana akanituma huko mbele ya . . . anaposema nami . . . kuna gogo la kale linalopakingama; huko mbali vilimani ambako nilikuwa nikitega nilipokuwa mvulana. Na humo ndani Yeye—Yeye akanijulisha nisiruhusu wasiwasi hata kidogo.

¹⁷ Basi nilipoenda nyumbani, nikapitia kwa Ndugu Wood (mtu aliye hapa pamoja nami, na dada), nilimwona maskini huyo jamaa mdogo akitoka nje kwenye baraza ya nyuma, uso wake mdogo ulionekana wa kijivu, naye alikuwa anaenda kumwaga maji machafu kwenye pi—pipa la takataka. Nami nikamwendea. Alikuwa akilia. Akasema, “Loo, Billy,” kasema, “Margie hata hawezi kunishughulikia.” Huyu ni yule nesi, nesi wa Mayo aliyeponywa katika mkutano wangu, akiwa na uzito wa pauni thelathini na tano, akiwa na kansa, kisa cha kwanza. Naye yuko kwenye kliniki ya kansa huko Louisville, amekufa kwa karibu miaka kumi; anauguza kwenye hiyo hospitali.

Kwa hivyo, kasema, “Margie yuko kwenye dharura, hawezi kunishughulikia.” Kasema . . . Anampenda sana.

¹⁸ Nikasema, “Angalia, Mpenzi, tunampenda Dada Margie, lakini hatumtegemei Dada Margie; tunamtegemea Bwana Yesu. Unaona?” Nikasema, “Tunampenda Dada Margie.” Kisha nikasema, “Nataka uwe na moyo hodari.”

Kasema, “Kwa nini?”

Nikasema, “Unajua nimekuwa wapi?”

Akasema, “Nina fununu.”

Nikasema, “Nina BWANA ASEMA HIVI.” Um-hum. Hilo lilitosha, mnaona, papo hapo.

¹⁹ Basi kesho yake asubuhi huyo mtoto mdogo akazaliwa. Ndipo yule nesi aliposhuka, sote tulikuwa kundi la akina baba, mnajua, jinsi wanavyopitia kwenye zulia, mnajua, kwa hiyo, papo hapo nikiandamana nao. Nesi akashuka, akasema, “Kasisi Branham?”

Nami nikasema, “Naam, mama.”

Akasema, “Ninakuonyesha mvulana mzuri, wa ratili saba na wakia tatu.”

Nikasema, “Joseph, umechukua muda mrefu kufika hapa. Lakini hakika nina furaha umewasili.”

Kasema, “Kwa nini umwite Joseph?”

Nikasema, “Huyo ndiye.”

²⁰ Ni vigumu sana kumwacha, kwa kuwa ameanza tu kujua kutembea hivi punde, akipiga kelele, “Wapi Dada?” Lakini ni majaliwa makubwa kufanya hivyo kwa ajili ya Bwana Yesu. Nami ninajua ninyi wanaume, wengi wenu hapa, vivyo hivyo, mna mambo. Lakini moja ya siku hizi tukufu, “nikiwa mwaminifu kwa Mwokozi wangu, nitaushikilia mkono Wake uongozao, Yeye atatuongoza kuuvuka huo mto.” Hilo ndilo jambo kuu.

²¹ Sasa, itabidi—itabidi mtoke mapema kidogo mpate kwenda nyumbani, na mle chakula chenu cha mchana, kisha mrudi. Nao watakuwa wakisambaza kadi za maombi kwa ajili ya usiku wa leo. Nanyi mliwazia nini kuhusu jana usiku? Mlipenda hilo vizuri zaidi? Basi, hilo ni zuri.

²² Nilishukuru sana kwa ajili ya usiku uliopita, mara ya kwanza ambapo nimekuwa nayo tangu mimi...kwa miaka na miaka. Ni wangapi wamehudhuria mikutano yangu katika maeneo mengine? Ninii tu...Mwajua, hiyo ni kweli. Nami...

²³ Huyu asingekuwa ninayemwazia kuwa, sivyo? Jim O’Neal, sivyo? Loo, jamani, je, Jimmy yuko hapa? Huh-uh. Nanii...Mtu huyu, Ndugu Green, mkwewe ndiyo sababu ninaweza kuendesha Ford, nanii wake...mkweo. Nami nashangaa tu kama Jimmy alikuwa hapa, mvulana mzuri wa Kibaptisti, nami bila shaka ninampenda.

²⁴ Nasi tu—tunajaribu kutoka mapema kidogo, ili kwamba hao wa—wavulana waweze kurudi na kuzisambaza kadi za maombi za alasiri ya leo. Nasi tunatarajia kumiminwa kukuu kwa baraka Zake, kama jana usiku.

²⁵ Nikiwa nimesimama hapa jana usiku, nilipokuwa na mstari wa kawaida, bila ule mwingine, (Mnaona?), na nikahisi, nilipoinua mikono yangu juu, juu ya, huo uvimbe na mafundo na kadhalika. Unahisi tu jambo fulani likitukia mkononi mwako, unaangalia, nao haukuwepo. Hiyo—hiyo inakufanya ujisikie una furaha. Nakwambia; kweli inakufanya; inanifanya nijisikie kurudi na kuwa na ibada za uponyaji.

²⁶ Huko kwenye ninii...Biblia hii ya kale iliyobarikiwa, ambayo ndiyo Kitabu cha mwongozo wa Uzima, wa Milele; na katika Ezekieli mlango wa 36, nasi tutasoma ninii...mstari mmoja tu kutoka kwenye m—mlango wa 36, kifungu cha 27. Na kwa ajili ya somo, ninataka kutumia, alasiri ya leo, *Uigaji Wa Ukristo*. Na Bwana na aongeze baraka Zake kwenye Neno Lake tunapolisoma.

Nami nitatia roho yangu ndani yenu,...mtazishika hukumu zangu, na kuzitenda.

²⁷ Sasa, Ezekieli alikuwa nabii, naye nabii katika Biblia alihebiwa kuwa tai. Sasa, tai ni ndege mwenye nguvu, naye anaweza kuruka juu sana kuliko ndege mwingine yeyote, kwa sababu ma—maumbile yake ni tofauti na huyo ndege mwingine. Anaweza kustahimili mwi—mwinuko wa juu, naye anaruka juu sana hewani. Naye Mungu alimfananisha nabii Wake na tai. Walifanyizwa tu hivyo. Wangepanda juu katika Roho na kwenda juu sana, nao wangeweza kuona mambo ya mbali yakija. Ndipo wanaposhuka, wangeweza kujua kilichokuwa kikifanyika.

²⁸ Naye Ezekieli alikuwa mmoja wa tai wa Mungu, ambaye angeweza kuruka juu kabisa na kuona mamia na mamia na... ya miaka ijayo. Unajua, ni kama kadiri unavyozidi kwenda juu ndi—ndivyo unavyoweza kuona mbali zaidi. Na hivyo ta—tai ana ji—jicho pevu la kweli la kuendana na mwinuko huo; kwa sababu kama hakuwa na jicho pevu, isingemfaa kitu kupanda juu, hangeweza kuona mbali sana. Lakini jicho la tai ni bora zaidi kuliko mwewe wakati wowote. Anaweza kuona mbali kuliko mwewe, kumshinda kuruka vyovyote atakavyo. Na yuko juu sana kuliko mwewe.

²⁹ Nami nimechunguza wanyama pori na—na ndege. Basi wakati mmoja nilikuwa Cincinnati, chini hapa, kwenye lile mbuga kubwa la wanyama. Wengi wenu mmekuwa huko. Nao walikuwa ndio kwanza wamshike tai, na kumtupa kwenye kizimba. Naye maskini ndege huyo, hakika nilimhurumia. Angeweza kurukia fito hizo kwa kila kitu alichokuwa nacho. Alipiga akayang'oa manyoya yakatoka kichwani mwake, akang'oa manyoya kutoka kwenye mbawa zake. Angejitupa ndani yake namna *hiyo*, akijaribu kuruka atoke. Naye akapiga hizo fito na kurushwa nyuma; akalala pale kichalichali. Macho hayo yangechungulia angani.

³⁰ Ndipo nikawazia, “Loo, maskini ndege huyo ni mwenye mashaka jinsi gani. Kwa maana alijengwa, akafanywa kuwa ndege arukaye mbinguni. Na hapa alikuwa amenaswa, kwa maisha yake yaliyosalia, katika kizimba kidogo.” Huku akijua ya kwamba angeweza kutazama na kuona mambo ambayo... na maeneo ambayo alitamani kuwa, lakini asingeweza kutoka nje ya kizimba hiki.

Nikawazia, “Ni mtu mwenye mashaka jinsi gani, au, ndege hana budi kuwa.” Nikawazia, “Hiyo ni karibu mojawapo ya tamasha za kusikitisha sana nilizowahi kuona.”

³¹ Lakini basi, nilipogeuka, niliona jambo la kuhuzunisha zaidi. Nalo hilo ni, wana wa Adamu, walioumbwa kuwa wana wa Mungu, wakigongesha akili zao, wakijaribu kutafuta anasa za kuridhisha katika maisha haya, huku wakijua kwamba walizaliwa wapate kuwa wana wa Mungu aliye hai; nao kwa urahisi wanajigongesha hata kufa, wakikimbia *huku* na kukimbia *kule*, na kupigana risasi, kucheza kamari, na kuiba, na kunyang’anyana, wakati kweli wamezaliwa kuwa wana wa Mungu. Hiyo ndiyo tamasha ya kuhuzunisha kuliko zote niliyopata kuona, ni watu waliotiwa kifungoni na dhambi.

³² Lakini kuna jambo moja kuihusu. Kunaweza kuwa na kitu kama mtu fulani mwenye fadhili kumwachilia huyo tai atoke mle. Nami nina furaha sana kuwaambia wana wa Adamu, alasiri ya leo, kwamba kumekuwako na Mtu mwenye fadhili aliyewajia wana wa Adamu: Bwana Yesu, atakayemweka huru kila mtu anayetaka kuwa huru. Ni juu yako.

³³ Sasa, tunaona watu wengi sana wakijaribu kuiga Ukristo. Ukristo ni...haumaanishi kujiunga na kanisa. Ukristo ni ujuzi. Mtu fulani ameniambia...vema, ilikuwa huko Little Rock, Arkansas. Tulikuwa katika Ukumbi wa Ukumbusho wa Robinson, nao watu walikuwa wamekusanyika na kujaa mitaani, naye Bwana alikuwa anatupa uamsho mkuu.

³⁴ Basi kulikuwa na ndugu ambaye alikuwa Mnazarayo, alikuwa jukwaani, naye alikuwa akiuza penseli mitaani. Naye alikuwa na magongo ambayo alikuwa ametembelea, kwa miaka mingi. Angesimama kwenye magongo yake huku amevua kofia yake na ana penseli za kuuza, ombaomba. Ndipo Bwana katika majaliwa ya Uungu Wake, hekima na neema kwa mwanadamu, akaonyesha ono, akamwambia kuhusu jambo fulani lililokuwa limetukia, ndipo huyo mtu akaponywa papo hapo. Basi kesho yake alikuwa na bango kubwa kwenye mikongojo akitembea mtaani, namna *hii*, akipakia huku na huku, akimwonyesha kila mtu. “Marafiki hawa wa kale walikuwa wakinisaidia kutembea. Sasa, ninaegemea kwenye mikono ya milele (Na alikuwa...) ya Bwana Yesu.”

³⁵ Na alikuwa na shauku kubwa sana. Basi aliporudi kwenye ibada usiku huo, alikuwa ameketi kwenye roshani, kitu kama hicho. Na vizuri sana ninavyoweza kukumbuka, una mbili au labda—labda roshani mbili au tatu. Na kwa vyovyote vile, nilikuwa ndio kwanza ninaanza kuzungumza kama sasa, naye alikuwa amechangamka sana, maskini huyo ndugu, mpaka akasimama, akasema, “Ndugu Branham, ninataka kukuuliza jambo fulani.”

Nikasema, “Naam, ndugu.”

³⁶ Akasema, “Nilikusikia ukihubiri, nami nikajua tu kuwa wewe ni Mnazarayo.” Kisha akasema, “Ndipo nakusikia... mtu mwingine akasema ulikuwa Mbaptisti.” Kisha akasema, “Halafu naona wote wanaokuzunguka ni Wapentekoste.” Kasema, “U nani wewe, Ndugu Branham?”

Nikasema, “Hiyo ni rahisi. Mimi ni Mbaptisti Mnazarayo wa Kipentekoste.” Kwa hiyo hilo ni sawa kabisa...

³⁷ Ukristo ni maisha. Pentekoste, ni—ni... Ninajua wameiundia dhehebu, neno *pentekoste*, na kulitumia tu hilo jina kwa faida yao. Lakini Pentekoste ni tukio, sio dhehebu. Pentekoste ni ya Wabaptisti, Presbiteri, Lutheri, Nazarayo, hao wote. Pentekoste ni tukio.

Na inaonekana kuwa baadhi ya watu wana wakati mgumu sana kujaribu kuishi maisha ya Kikristo, wakati kweli, sio hivyo, ni...

³⁸ Mtu fulani alisema, nilipotoka katika jaribu langu kuu wakati huo, baada ya kumpoteza mke wangu, mtoto mchanga, na kila kitu, kasema, “Ndugu Branham, je, uliidumisha dini yako wakati huo?”

³⁹ Nikasema, “La, bwana, ilinidumisha wakati huo.” Kwa hiyo hiyo ndiyo kazi yake. Siwezi kumdumisha Kristo; Yeye ananidumisha. Sio kama nilishikilia; ni kama Yeye alishikilia. Na ni zawadi kwangu.

⁴⁰ Na halafu wakati, tukiona kwamba watu wana wakati huu mgumu, hapana shaka kuna kasoro mahali fulani. Sasa, ikiwa dini ya Kikristo inajumuisha tu azimio la kununi ya imani, dhehebu, au kiakili, basi hatuhitaji chochote ila kundi zuri sana la watu wewevu. Hilo ndilo tu tunalohitaji, kama kanisa litatawaliwa na mtu mwenye akili.

⁴¹ Sasa, mambo ya kiakili ni sawa. Unaweza kulipokea Neno kiakili, lakini liache lizame moja kwa moja hadi moyoni. Hapo ndipo li—linapoanza kupata matokeo.

⁴² Sasa, lakini kama Mungu alitukusudia sisi kuliendesha kanisa Lake kwa madhehebu ama kwa kanuni za imani, basi jambo pekee tunalohitaji ni akili ya mwanadamu: kadri mtu alivyo mwenye akili zaidi, ndivyo kanisa linakuwa bora. Lakini huo haukuwa mpango wa Mungu. Mpango wa Mungu ulikuwa ni Roho Mtakatifu kuliongoza kanisa. Roho Mtakatifu alitolewa kwa ajili ya kanisa. Wala hatuwezi kuwa na mamlaka mbili zikiendesha kanisa kwa wakati mmoja. Mwanadamu akiliendesha, Roho Mtakatifu huondoka. Roho Mtakatifu akiliendesha, kwa kawaida mwanadamu huondoka. Kwa hivyo ni mmoja au mwingine.

⁴³ Kwa hiyo, hatuna budi kufikia uamuzi huu, kwamba, Mungu anamkusudia Roho Mtakatifu kuliongoza kanisa. Sasa, simaanishi kwamba Roho husimama tu na ukihubiri, kwa

sababu Roho Mtakatifu huwaweka watu kanisani kwa ajili ya jambo fulani; lakini ninamaanisha, kama wa kiakili ndio tu wanaohitajika.

⁴⁴ Angalieni, sasa hapa, Ezeieli akizungumza, alisema jinsi ambavyo angeweka moyo mpya (mlango uo huo), auondoe ule moyo wa kale, wa mawe, Naye angekupa roho mpya. Halafu basi angeweka Roho Yake ndani yako.

⁴⁵ Sasa, roho mpya haimaanishi kuukarabati ule wa kale. Haimaanishi kwamba kanisa linahitaji ukarabati. Inamaanisha kanisa linahitaji kuzaliwa. Kanisa la Mungu halihitaji kupigwa msasa; linahitaji uongofu. Hiyo ni kweli. Basi kuchukua tu kanisa la kale na kuketi, kusema, “Vema, nawaambia, tutabadilisha halmashauri ya mashemasi. Tutabadilisha wachungaji.”

Hicho sicho kanisa linachohitaji. Linahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu. Linahitaji nguvu za Mungu aliye hai.

Uamsho haumaanishi kutoka nje na kupata wafuasi wapya, *uamsho* unamaanisha, “kuamsha kile ulicho nacho tayari.”

⁴⁶ Hapa si muda mrefu uliopita, nilipata tukio la ajabu sana kuhusu hilo huko Chicago. Nilikuwa nimesimama kando ya ziwa kuu, Ziwa Michigan, nami nikaona mawimbi yakiruka hewani, na povu likiruka, na loo, lilikuwa na wakati wa jinsi gani, likizirusha maskini meli hizo ndogo huku na huku. Ndipo nilipolitazama, niliwaza, “Unafurahia nini sana? Una uamsho.” Lakini nikawazia, “Unajua nini? Unaweza kuwa unaruka na kupiga makelele huko nje, lakini huna hata tone moja zaidi la maji ndani yako, kuliko uliyo nayo unapokuwa mtulivu kabisa. Hiyo ni kweli; maji yale yale tu, ni kwamba tu umepata uamsho.”

⁴⁷ Sasa, uamsho unahitaji nini? Unahitaji upepo kuja, uanze kuvuma. Huo ndio kanisa linaohitaji: ni baadhi ya Upepo ule ulioshuka Siku ya Pentekoste, ushuke kasi na kuliamba; si Mbaptisti mpya, si Mmethodisti mpya, bali uamsho katika Wabaptisti na Wamethodisti. Na huko kurusha maji kunafanya nini huko nje? Ni—ni kwa kusudi fulani. Hufagilia takataka zote ukingoni kutoka majini. Hivyo ndivyo uamsho unavyofanya, kwa namna fulani unapiga na kuondoa tofauti zote kutoka kwetu, tukimruhusu Roho Mtakatifu atupige. Ndipo inaleta tofauti kubwa sana, inasafisha, inayasafisha maji, basi.

⁴⁸ Sasa, huwezi tu kuwa na wakati wa kupiga msasa kanisani kama uamsho. Nami natumaini ya kwamba baada ya mkutano huu, ya kwamba kutakuwako na uamsho kila mahali katika jiji hili; natumaini, na nchi nzima. Nafikiri ni wakati wa uamsho. Nao uamsho huu mkuu tunaozungumzia hauna budi kutoka Mbinguni. Hauwezi kuja kwa njia ya mwanadamu. Haukuzaliwa na mwanadamu. Umezaliwa na Mungu, na hauna budi kutoka kwa Mungu. Wala huwezi kuuweka uamsho huu katika theolojia

ya kale na kuuchanganya. Yesu alisema hivyo katika Luka Mtakatifu: “Huwezi kutia divai mpya katika viriba vikuukuu.”

⁴⁹ Mara nyingi nilishangaa ni kwa nini tamshi hilo lilitolewa, kwa nini huwezi kutia divai mpya katika viriba vikuukuu? Nikaja kugundua kwamba... Nilisema, “Sikilizeni hapa, tuna gudulia la glasi, ama chupa, kwa nini nisingeweza kutia divai mpya mle ndani kama vile nilivyoweza kutia divai ya kale ndani yake.”

⁵⁰ Lakini nikagundua ya kwamba huko nyuma katika siku ambazo Yesu alikuwa akizungumzia, vile viriba havikutengenezwa kwa glasi. Hawakuwa na watengenezaji wa vifaa vya glasi siku hizo. Navyo vilitengenezwa kwa ngozi ya mnyama. Nayo hiyo ngozi ya mnyama ilikuwa imetengenezwa na kushonwa, au, kufungwa, na wakatia di—divai, maji, vitu vya majimaji katika kiriba cha ngozi. Ndipo baada ya kiriba hicho kuwa kikuukuu sana, mpaka hicho... hakuna divai ndani yake wala chochote kile, kilikauka. Mafuta ya wanyama ya ngozi yalitoka. Na kisha ikawa ngumu na kavu kabisa.

⁵¹ Nami ninaona kile Yesu alichomaanisha, basi: ukitia divai mpya, isiyochachuka, katika kiriba kama hicho, na hiyo divai mpya ilikuwa na uhai ndani yake, nayo ikaanza kufanya kazi na kuchachuka, ingekipasua hicho kiriba. Na hivyo ndivyo unavyouchukua ubatizo wa Roho Mtakatifu na kuuweka katika ngozi kuukuu, kavu, baridi, ya ng’ombe, italipuka bila shaka. Huwezi kuihifadhi hivyo.

⁵² Ukijaribu kuchukua ubatizo wa Roho Mtakatifu pamoja na maskini tukio la kale la ujuzi fulani wa kanisa wa muda mrefu, hakika utapasuka bila shaka. “Lakini divai mpya,” alisema Yesu, “hutiwa kwenye viriba vipya.” Viriba vipya vingali vina mafuta ya mnyama ngozini, na ni rahisi kunyambulika. Hivyo ndivyo kanisa la Mungu linavyopaswa kuwa kwa ajili ya uamsho: kunyambulika.

⁵³ Unajua, ungeweza kutia Divai mpya, ambayo inawakilisha Neno, kutia Divai mpya katika kiriba kikuukuu, nawe utalisoma Neno, Nalo linasema, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele.”

Kiriba cha kale kitafanya, “Puuf!” kipasuke: “Siliamini.”

“Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni halisi tu siku hizi kama ulivyowahi kuwa”: “Puuf! Siamini hilo.”

⁵⁴ Nawe unafanya nini? Unaharibu kiriba na divai pia. Unatupa lulu mbele ya nguruwe. Ujumbe wako umesambaratika, wala hakuna wa kuupokea, vililipuka tu navyo... hakuna lingine kwake. Lakini ukichukua viriba vipya na kuweka Divai mpya ya Roho Mtakatifu ndani yake, nalo Neno linasema... Linafanya kazi hai moyoni, na Hilo linasema, “Yesu Kristo ni yeye yule jana na hata milele.” Divai inasema, “Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

Kiriba kipya kilisema, “Amina!” kinanyambuka.

⁵⁵ Kasema, “Yesu Kristo alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa, ni yeye yule tu jana, leo na hata milele.”

Kiriba kipya kinasema, “Amina!” Kinaenea kwa maisha mapya. Vyote viwili vinawekwa na kuhifadhiwa. Kwa hivyo huwezi kutia divai mpya kwenye viriba vya kale.

⁵⁶ Katika Siku ya Pentekoste, Mungu alikuwa na viriba vipya kabisa, vya Kipentekoste mia moja na ishirini, vimeketi huku vimeinua shingo zao. Ndipo Roho Mtakatifu aliposhuka kutoka Mbinguni, alivijaza viriba hivyo, navyo vikarukaruka kila mahali, vikihubiri Injili kwa ulimwengu uliojulikana, wakitangaza kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Liangalieni.

⁵⁷ Hapa siku moja nilipata tukio. Nilikuwa huko juu katika misitu ya kaskazini, mbali katika British Columbia. Nami nilikuwa nimefanya mikutano kadhaa huko juu miongoni mwa Wahindi na watu katika nchi hiyo. Ndipo mmoja wa watu waliojua kwamba nilipenda kuwinda sana, alisema, “Billy, ungependa kufanya safari ya kuwinda huko nyuma milimani baada ya mikutano?”

Nikasema, “Hakuna kilicho bora zaidi.”

⁵⁸ Kwa hiyo tukawachukua farasi ishirini na mmoja, na kuwapakia, nasi tulikuwa maili elfu moja mia moja kutoka kwenye barabara ya lami na kama maili mia mbili kutoka kwenye iliyosakafiwa, tukiwa na farasi ishirini na mmoja, huko nyuma tukiwinda mbuzi wa milimani.

⁵⁹ Basi nakumbuka siku moja... Ninapenda tu mambo ya mwituni; huko ndiko unakompata Mungu, ikiwa tu utakuwa peke yako katika maumbile, unaweza kumwona. Nami nilikuwa nikimfuatilia maskini dubu mkubwa mkali. Sikumtaka, kwa sababu sikuwa na pesa, za kutosha, kununua kibandiko cha kumbeba. Lakini nilitaka tu kumwangelia. Nami nikamfukuza kutoka kilima hadi kilima juu ya maskini farasi wangu mdogo. Nami nilikuwa na shida nyingi sana na maskini farasi huyu; alikuwa tu mwenye umri wa miaka mitatu, na aliazimia kunitupa. Na kwa hivyo, angesimama mara kwa mara na kuangalia tu jinsi angeweza kufanya onyesho zuri kwake. Na kwa hiyo tungezunguka-zunguka hivyo vichaka mbio.

⁶⁰ Nami ningemchochea kasi kupanda kilima zaidi na zaidi. Ndipo hatimaye, nikachanganyikiwa. Nikawazia, “Sasa, ni ipi mashariki na magharibi sasa?” Kwa hivyo nikawazia, “Sasa, ngoja. Hutaki kuchanganyikiwa huko juu.” Kwa sababu unaweza tu kwenda mbali sana bila kupata chochote. Kusema kweli, mtegaji alienda mara moja kwa mwaka kwenye barafu wakati aliposhuka mpaka kwenye mto, unaoitwa Mto wa Misonobari ya Mashariki.

⁶¹ Kwa hiyo basi nikawaza, “Sasa, nilipitia njia gani?” Nikawazia, “Kama nitapanda mlima mrefu zaidi...” Basi kulikuwa kukinyesha, ukungu kidogo bondeni. Kwa hivyo nikawazia, “Labda huenda nikapata mwelekeo wangu.”

⁶² Nikipanda barabarani, nilishika mwelekeo wangu, lakini nikaona ilinibidi nigeuke na kupitia njia nyingine. Nilichelewa sana kuingia. Nami nikawazia, “Bwana...” Nikiwa nimepanda farasi wangu kule na kumsifu Mungu kwa kuwa peke yangu, nikawazia, “Loo, ni vizuri sana kuwa peke yako msituni.” Nalipenda tu hilo. Na ni...

⁶³ Dhoruba zilikuwa zimepita na mwezi ulikuwa umechomoza baada ya jua kutua. Nao mwezi ulikuwa unang’aa na halafu kukawa na mawingu meupe, ninayoita “anga za mtindi,” kama tu malundo makubwa ya mawingu yakipita. Basi nilipokuwa nikienda kwa farasi; nilisimama. Kitu fulani kilionekana kunitia moyo kusimama. Kwa hiyo nikasimama na kumfunga farasi wangu mdogo, kwa sababu alikuwa akitoa mapovu sana. Nami nikapanda gogo na kuketi chini.

⁶⁴ Ndipo nikatazama juu angani, nikasema, “Ee Bwana Yehova, Wewe ni mkuu sana na wa ajabu sana. Jinsi ninavyokupenda Wewe.” Ndipo nikaanza kusikia kelele za ajabu, za uchovu sana. Na ni kelele za maombolezo, kitu tu ambacho kingekufanya kidogo ujisikie, kama vile tungenema katika usemi wa mitaani, kwa namna fulani kimizuka.

⁶⁵ Ndipo nikatazama huku na huku, nami nilikuwa karibu na teketezo la kale. Sijui kama mnajua teketezo ni nini au hamjui. Ni mahali ambapo mioto ilipitia miaka mingi hapo awali na kuteketeza maganda yote ya miti, nayo inasimama pale tu. Ndipo wakati hilo jua, ama, mwezi, hasa, unapochomoza nyuma ya mawingu, na kwenye hizo pao nyeupe zilizopauka, miti, iliyosimama, ilionekana kama mawe ya kaburi. Nao upepo ukavuma, huku mawingu yakipita juu kasi, ulitoa sauti ya maombolezo: “Wooi!”

⁶⁶ Nikawazia, “Ee Mungu, kwa nini uliniweka mahali kama hapa? Hapa ni mahali pabaya sana kuwapo hapa.” Nami nikatazama pande zote, na maombolezo yote na kuugua kwote nilikopata kusikia: kupiga makelele, kuomboleza. Upepo unavuma na miti hiyo ikiomboleza katika huo upepo, nikasema, “Bwana, sikuzote nilijua kuwa uliishi msituni, basi ni kwa nini nilivutiwa kusimama mahali hapa? kwa kuwa hapa panaonekana kama mahali pa kutisha sana.”

⁶⁷ Basi nilipokuwa nimeketi pale, kuna Andiko lililonijia niani mwangu, nalo lilikuwa katika Yoeli. Lilisema, “Kilichosazwa na tunutu, kimeliwa na madumadu; na kilichosazwa na madumadu kimeliwa na nzige.” Kuendelea, wadudu mbalimbali wamekula uhai wote kutoka kwenye huo mti.

⁶⁸ Ndipo nikawazia, “Naam, hiyo ni kweli. Nami hapa nimesimama karibu na hiyo miti. Wakati mmoja ilikuwa ni miti mikubwa iliyosimama hapa. Ndipo upepo ulipovuma katika siku zilizopita, ilichezacheza huku na huku katika wadhifa wao mkuu wa kifalme; ilisogea kifalme huku pepo zikiipeperusha, lakini loo, sasa ni tofauti jinsi gani.” Jambo fulani lilikuwa limetukia. Loo, naam, ilikuwa ni miti bado. Hiyo ni kweli. Lakini jambo fulani lilikuwa limetukia. Mkondo wa utomvu, mkondo wa uhai wa mti ulikuwa umeteketewa, ukaondolewa.

⁶⁹ Basi nikawazia, “Vema, hii ina maana gani?” Ndipo nikaanza kuwazia, basi, juu ya mahali nilipokuwa, na watu waliokuwa... Nilikuwa nimesikia wakipinga na kusema kwamba siku zote za miujiza zimepita. Nami nikawazia, “Hiyo ni kweli. Hiyo ni kama tu baadhi ya makanisa haya makubwa mno yenye minara-pia yanayosimama na majina makubwa nyuma yao, majina ya kihistoria, kwamba, ‘Wakati mmoja tulikuwa *hivi-na-hivi*; tulikuwa *hivi-na-hivi*.’” Lakini Mkondo wa uhai umekatwa.

⁷⁰ Madhehebu, tangu wakati wa yale matengenezo ya kwanza na waanzilishi wao, kundi jipya la waalimu liliingia na kukata ule Uzima halisi wa Roho Mtakatifu. Nao waliyumbishwa na upepo wa nguvu ukienda kasi kama ulivyokuja kwenye Siku ya Pentekoste. Lakini sasa, wakati Mungu anapotuma upepo Wake kila mara, nao unashuka kwa ngurumo, kitu pekee wanachoweza kufanya ni kuomboleza: “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mambo haya yote yamepita.”

⁷¹ Ni mahali pa kimizuka jinsi gani kuwa. Na nikawazia, “Loo la, hapana shaka ilikuwa ni miti; ilikuwa na historia nyuma yake kama miti; lakini uhai ulikuwa umeiacha.”

⁷² Na hiyo ndiyo shida ya Wapentekoste wetu, Presbiteri, Methodisti, Baptisti, Nazarayo, Pilgrim Holiness: wadudu wa kimadhehebu wamekula Uhai kutoka kwake, nalo limekuwa tu mnara-pia mkubwa, wa kale, uliokufa. Tunachohitaji ni uvumi mkubwa wa upepo wa nguvu ukienda kasi na Mkondo mpya wa uhai wa kuupokea; kweli.

⁷³ Loo, msinielewe vibaya. Silihukumu kanisa wala madhehebu; ninahukumu kutokuwepo kwa Kristo katika maeneo haya. Na kitu pekee kinachowafanya waugue na kuomboleza wakati Mungu anapotuma uamsho wa Roho Mtakatifu ulimwenguni ni kwa sababu ya ukosefu wa Uhai unaonyambuka ndani yao kuupokea. Roho Mtakatifu alishuka kwenye Siku ya Pentekoste, kwa yeyote ambaye angeamini angempokea.

⁷⁴ Petro alisema, katika Matendo 2:38, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa

kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Na kama Mungu angali anaita, Roho Mtakatifu angali anashuka. Hana budi kushuka.

⁷⁵ Kwa hivyo nikiwa nimekaa kwa mshangao, nikitazama, niliwaza, “Vema, ni nini kilichosababisha hii? Ni nini kilichouondoa ule uhai? Yaliyosazwa na Walutheri, yameliwa na Wamethodisti; yaliyosazwa na Methodisti, yameliwa na Baptisti; yaliyosazwa na Baptisti, yameliwa na Wanazarayo; yaliyosazwa na Wanazarayo, yameliwa na Wapentekoste.” Basi ndugu, hatuna kitu ila jina tu la kanisa. Basi nikawazia, “Si ni jambo fulani hilo? Si ajabu kuna uigaji mwingi sana wa Ukristo; si kitu ila ni dhahaka.”

⁷⁶ “Sitaenda kwenye jengo lile. Hapana, nisingeshirikiana na kitu kama hicho.” Um-hum. Ukosefu wa Uzima, hivyo tu, si ukosefu wa kanisa, ukosefu wa Uzima.

⁷⁷ Ndipo nikasema, moyoni mwangu, kwa Mungu, nikasema, “Kwa nini ungali unatuma upepo basi?” Ndipo mawazo yangu yakaingia katika Maandiko, giza mno nisingeweza kusoma Agano langu dogo mfukoni mwangu. Lakini nikasema, “Kwa nini utume upepo?” Ndipo mawazo yangu yakaendelea kushuka chini, yale Maandiko, lakini alisema chini yake tu, “Nitarudisha, asema Bwana. Yote yaliyoliwa na madumadu, yote yaliyoliwa na nziige, nitayarudisha.”

⁷⁸ Halafu basi nikashangaa, nikitazama nje katika kuanguka kwa zile koni za miti hii na mbegu zao tofauti, chini ardhini, si virefu sana, wala si vikubwa sana, lakini kulikuwa na vichaka vikichipuka, miti mipya ikichipuka. Ndipo pepo zilipovuma, vilicheza-cheza tu, na kutikisika, na kuruka, na kutetemeka, na kuendelea. Nikasema, “Endapo huo si uamsho wa mtindo wa kale, sijapata kuona mmoja. Hao ni watoto wa Mungu wakifurahi tu na kucheza-cheza katika baraka za Mungu wakati zikimiminika chini.”

⁷⁹ Vema, Jambo fulani likanijia, kasema, “Hiyo ni ya kijani kibichi. Ni michanga na ya kijani kibichi.” Afadhali niwe mchanga na wa kijani kibichi, na niweze kunyumbulika, niwe na uhai, kuliko kuwa mzee, na kushupaa, na nimekufa, na bila ya chochote. Kwa hivyo hata moto kidogo wa porini, badala ya kutokuwa na moto hata kidogo.

⁸⁰ Basi upepo ulipovuma, hiyo miti midogo ilicheza-cheza na ikawa tu na uamsho mkubwa wa Kipentekoste wa mtindo wa kale. Nami nikawazia, “Kwa nini unafanya hivyo basi? Si ingechipuka tu vile vile kama usingekuwa na mabatizo haya yanayowaangukia na kuwatikisa? Nayoy... Je, hiyo si ni miti vile vile tu?”

⁸¹ Lakini Kitu fulani kinaniambia moyoni mwangu, “Naam, lakini kila wakati ninapoitikisa, ninailegeza mizizi ipate kuingia

kwa kilindi zaidi.” Hivyo ndivyo uamsho mkuu unavyofanyika mjini.

⁸² Sasa, miamsho hii mipya ya Kipentekoste ni nini? Si kitu ila mazao kutoka kwenye mti wa kale. Pale hasa ambapo miti ya kale ilipokufia, Mungu alikuwa na njia ya kuleta uhai tena. Kama vile tu tunapozeeka na kufa, Mungu humwinua mtu mwingine kwa sisi kama mti, mzao, ama chochote kile. Tunachukua Biblia ile ile waliyosoma.

⁸³ Vipi kama baadhi yenu Wamethodisti...aibu kwenu, nilikuwa tu nikisoma baadhi ya maandishi ya John Wesley. Na ambapo, alipokuwa huku pamoja na Asbury, naye alikuwa amempanda farasi wake siku moja, naye huyo farasi akaanguka na kuvunja mguu wake. Basi Wesley alishuka, akatoa mafuta yake mfukoni mwake, na kumpaka farasi wake mafuta, akampanda, akaenda zake.

⁸⁴ Kwa nini hamwezi kushirikiana katika uamsho wa uponyaji? Ikiwa Mungu anaweza kumponya farasi, hakika anaweza kumponya mwanadamu. Kuna nini? Waalimu wenu wachanga, wapumbavu wamewapulizia wakawajaza dawa ya kufanya maiti isioze, na hiyo ndiyo sababu hamwezi kuishi. Hiyo ni kweli.

⁸⁵ Ati Wabaptisti? John Smith alilia na kuomba kwa ajili ya uamsho hadi macho yake yakafunga, mpaka mkewe angemwongoza mezani kula chakula chake. Angesema nini kwa kanisa letu la Kibaptisti kama angefufuka? John Smith angesema nini kufufuka na kulitazama kundi la utakatifu? Wakati wao...yeye alihubiri mahubiri yake ya mwisho akiwa na umri wa miaka themanini na kitu, naamini ndivyo ilivyokuwa. Walimbeka kumpeleka mimbarani, wala hakuhubiri, mafupi tu: saa nne. Nanyi hamwezi kustahimili dakika ishirini. Hakuna Uhai wa kuupokea ule Upepo hayo tu.

⁸⁶ Naye akasema, “Moyo wangu unavunjika sana kuona binti zetu wa Kimethodisti wakivaa pete za dhahabu kwenye vidole vyao.” Angesema nini sasa akiwa amevaa maskini kaptura za hatamu? Huo ndio ukweli. Nao huenda ukakuboresha na kukuchefua.

⁸⁷ Nilipokuwa mvulana mdogo, hatukuwa na chakula kingi, huko chini milimani. Mama alikuwa akichukua ngozi za nyama kutoka kwa duka la mboga, na kuziweka kwenye karai kubwa ya kale, ya mikate, na kuzichemsha, ama, kuzichoma, apate mafuta ya kutengeneza mkate wa mahindi. Tulikuwa na mbaazi jicho nyeusi na mkate wa mahindi. Nyie wa kaskazini hamjui mlo mzuri ni nini.

⁸⁸ Kisha wakati ungeninii...wakati tungepata hicho...Na kisha kila Jumamosi usiku tulikuwa na beseni kubwa ya mbao, na birika la chai likiwa jikoni. Basi mtu mmoja angeoga, unaongeza tu maji, ndipo anayefuata anaoga, mpaka watoto wote walipooga, na kisha dozi ya mafuta ya mbarika. Nami

nilichoshwa tu na kitu hicho; hata nisingeweza kuvumilia harufu yake, bado. Nisingetaka mmoja wa watoto wangu anywe mafuta ya mbarika.

Ningemjia mama, na ningeshika pua yangu, nami ningelia. Ningesema, “Mama, kitu hiki kinanichefua sana.”

Angesema, “Lakini kisipokuchefua, hakikufai kitu.”

⁸⁹ Kwa hivyo labda nitatumia hilo kwa ujumbe huu. Labda itasababisha ulaji bora, tukinena kiroho, kuchochewa, kukufanya uombe urudi mahali unapopaswa kuwa.

⁹⁰ Naam, angalia utaratibu wa Maandiko. “Nitaondoa moyo wa kale wa mawe, na nitakupa moyo mpya.” Huo ndio utaratibu wa kwanza. Baadhi yao hukomea kwenye utaratibu huo wa kwanza. Sasa, hiyo ni kusema, wewe...ndio kwanza unaanza. Kisha akasema, “Nitakupa roho mpya.”

⁹¹ Hapo ndipo wengi wenu Wapentekoste mnaposhindiwa. Hum. Ilibidi uwe na roho mpya. Loo, ulijisikia vizuri na ulijisikia hivyo, “Loo, vema, mimi tu, loo, ninajisikia vizuri. Na—na—naachana na tabia yangu.” Vema, ndio kwanza umeanza. Unajiandaa tu sasa kuipata. Ndiyo kwanza unaingia tu mstarini. Ilimbidi kukupa roho mpya. Kwa nini usingeweza kupatana na roho yako ya kale; kwa hivyo unawezaje kupatana na Roho wa Mungu? Kwa hiyo ilimbidi akupe roho mpya.

⁹² Sasa, angalia Biblia. “Nitakupa...nitakuondolea roho ya kale, ya mawe, na kukupa moyo wa nyama: moyo mwororo. Na kisha nitakupa roho mpya. Halafu, nitaweka Roho Yangu ndani yako.”

⁹³ Sasa, angalieni. Roho Yake ilikuwa tofauti na roho yako mpya. Nao watu wengi wanapata roho mpya na kudhania wamepata Roho Mtakatifu. Wanaanza kujisikia wenye furaha, na kurukaruka, na labda wafanye mambo machache kidini. Nao wanafikiria ya kwamba wana Roho Mtakatifu, hata hivyo. Loo, hapana! Roho Mtakatifu anakufanya utende tofauti. Roho Mtakatifu hukufanya uwazie tofauti. Roho Mtakatifu aliwekwa moja kwa moja katikati ya roho yako mpya. Nayo roho yako mpya ikawekwa katikati ya moyo wako mpya. Moyo mpya, roho mpya, katikati ya moyo mpya, naye Mungu akasema, “Nitaweka Roho Yangu ndani yako.”

⁹⁴ Sasa basi, Roho wa Mungu anakaa moja kwa moja katikati ya roho yako, roho yako mpya. Na halafu si lazima utoke nje na kutenda kama Bibi Jones anavyofanya na kama Bw. Jones anavyofanya. Kuna kitu tu ndani yako; una upendo wa Mungu chini kabisa ndani yako, mpaka unauishia tu. Sio wewe; ni kitu Fulani ndani yako.

⁹⁵ Watu wengi hujaribu kujivika uso wa Kikristo au sura ya Mkristo siku ya Jumapili. Ndipo Jumatatu mnapaswa kuona uso

walio nao. Lakini sasa, huo ni uigaji, ambao si kitu ulimwenguni, katika kitabu changu, bali wanafiki. Kweli kabisa.

⁹⁶ Kama vile Mbunge Upshaw, kama nyote mjuavyo, alieponywa katika mikutano yangu baada ya kuwa mlemavu kwa miaka sitini na sita, alisema, “Huwezi kuwa kitu usicho.”

⁹⁷ Na hiyo ni kweli. Kuwa kile ulicho. Mungu aiialie siku, ambayo, wakati kanisa la Kikristo litakapokuwa kile linachopaswa kuwa. Ikiwa wewe ni wa Kristo, mwishie Kristo, toa yako yote kwa Kristo. Fungua moyo wako. Usiyawazie mambo yaliyo karibu nawe. Wazia jinsi Kristo alivyo kwako na ndani yako.

⁹⁸ Hiyo roho mpya ndani yako, na Roho Mtakatifu wa Mungu akikaa katikati ya roho yako mpya, ni kama tu springi kuu katika saa maarufu. Wakati spri—springi katika saa maarufu inapoanza tu kupiga, inafanya kila sehemu ya hiyo saa kufanya kazi sawasawa kabisa; ni hiyo springi mpya, springi kuu.

⁹⁹ Nayo springi kuu ya Ukristo ni ubatizo wa Roho Mtakatifu; si theolojia fulani iliyobuniwa na mwanadamu, si madhehebu fulani, bali ni ubatizo wa Roho Mtakatifu ambao hufanya kila kiungo katika Kanisa hilo kufanya kazi kwa utaratibu. Kuna kasoro, ndugu. Kweli.

¹⁰⁰ Jinsi tu Roho Mtakatifu anavyotenda kazi, Yeye hulitawala Kanisa Lake; kila pigo dogo huenda sawa kabisa, nalo hupiga kwa wakati halisi na Biblia. Kila kitu hupiga moja kwa moja kwenye Biblia; haijalishi mwanatheolojia anasema nini; Biblia inasema. Kinapiga moja kwa moja pamoja na hiyo, maana Roho Mtakatifu Ndiye aliyelandika Biblia, anaingia kuipiga Biblia maishani mwako, jinsi tu ilivyoandikwa. Loo, natumaini unaona hilo. Unalionga?

¹⁰¹ Sio kwa sababu unajisikia vizuri ukiwa na roho mpya, sio kwa sababu ulisafisha unywaji wako pombe na kadhalika; hiyo ni sawa, lakini. . . Si kwa sababu uliruka, au ulipaza sauti, au ulinena kwa lugha, ama ulijiunga na kanisa, ama njia yoyote ile. . . jambo la kidini ulilofanya, hilo halina uhusiano wowote nalo. Yesu Kristo alisema, “Kwa tunda lao mtawatambua.” Tunda la Roho ni upendo, furaha, fadhili, upole, subira, uvumilivu, imani, kiasi, sifa hizi zote nzuri ambazo ulimwengu unatarajia kuziona katika kanisa la Kikristo. Waliweka darubini ya Biblia ya Mungu kwa Wabaptisti, Wamethodisti, Pentekoste, Wanazarayo, na pande zote. Wanazitarajia hizo.

¹⁰² Paulo alisema, “Nijaponena kwa lugha za wanadamu na Malaika, nijapotoka na kuwaponya wagonjwa au kuhamisha milima na kadhalika, wala sina upendo wa kuunga hilo mkono, si kitu mimi.” Roho Mtakatifu ndani yako huyapiga maisha yako; ndipo nira inakuwa rahisi.

“Loo,” mtu fulani anasema, “Ndugu Branham, laiti ningaliweza kuishi Maisha hayo.”

“Loo, huna haja ya kuwa na wasiwasi kuhusu hilo, ndugu. Si wewe, kwa vyovyote vile. Ni Roho Mtakatifu ndani yako.”

¹⁰³ Paulo alisema, “Si... Maisha niliyo nayo sasa, si mimi, bali Kristo anaishi ndani yangu. Maisha ninayoishi sasa...” Kumbukeni, wakati mmoja alikuwa mtu wa kidini. Bila shaka alikuwa; msomi. Naye alikuwa mtu ambaye alijua Maandiko yote. Naye aliketi chini ya Gamalieli, mmoja wa hao, mmoja... waalimu mashuhuri sana wa siku hizo; labda mojawapo ya seminari bora zaidi za siku hiyo. Lakini alisema ilimbidi kusahau yote aliyowahi kujua ili kumpata Kristo, Roho Mtakatifu.

¹⁰⁴ Basi ungesema, “Lakini jirani yangu angeniambia, ‘Wewe ni mtakatifu anayejibingirisha.’” Loo, hilo jina la aibu ambalo shetani alilibandikia Kanisa la Mungu.

¹⁰⁵ Nimesafiri bahari saba, kwa neema ya Mungu, na kuhubiri karibu kote ulimwenguni. Nami niko katika milioni ya pili ya watu niliowaongoza kwa Kristo, kwa neema ya Mungu, wala sijapata kumwona mtakatifu anayejibingirisha bado. Katika dini zote za ulimwenguni sijapata kumwona mtakatifu anayejibingirisha. Ni jina chafu tu ambalo shetani humbandikia mwaminio.

Kasema, “Ati Mwaminio? Mimi ni mwaminio.”

Vema, tutatafuta kujua. Yeye alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Lichunguze kwa Neno.

¹⁰⁶ Sasa, angalia, huwezi kustahimili mateso. Sasa, sikiliza, rafiki, unajua siko hapa kukukemea. Niko hapa kukupenda. Niko hapa kukwambia ukweli. Nami naamini hiyo ndiyo sababu Roho Mtakatifu anaruhusu mambo haya yatendeke mikutanoni. Hiyo ni karama ya Kiungu, lakini hiyo haininii...Huo ni uthibitisho tu wa kitu fulani.

¹⁰⁷ Sikilizeni, niko hapa kuwasaidia, si kuwadharau au kuwadhihaki. Nisingefanya hivyo, hata kidogo. Lakini lazima uwe na maisha haya mapya. Na sababu ya kukuta watu wanaokuja madhabahuni kisha unawaona katika... Nitachukua kanisa langu mwenyewe, kanisa la Kibaptisti. Wanakuja, na kufanya maungamo, na kisha wanabatizwa, halafu unawaona katika majuma machache katika hali ile ile ya kale.

¹⁰⁸ Billy Graham, anayejulikana sana, anayejulikana ulimwenguni kote; njia zetu zimekutana mara nyingi, katika nchi za ng'ambo. Hivi majuzi tu huko Zurich, Uswisi, alimalizia kwenye uwanja wa michezo Jumamosi alasiri, nikaanza Jumapili asubuhi. Muujiza wa kisasa wa siku hizi, mtu wa ajabu, Mkristo halisi, nami nampenda mtu huyo na kumwombea, kwa maana haonekani kwangu kuwa mwanatheolojia mjuaji mwenye kiburi. Na, bali yeye ni mkweli na thabiti kwenye Neno, kadiri anavyoruhusiwa kuhubiri.

¹⁰⁹ Sasa, nilimwona katika kazi yake, na si muda mrefu uliopita nilipata fursa ya kuzungumza naye. Nami nilikuwa kwenye mkutano ambapo nilimsikia akitoa tamshi kama hili (Ilikuwa kwenye kiamshakinywa, ilikuwa, huko Louisville, Kentucky, miezi michache iliyopita.): Na kitu kuhusu, alisema, “Biblia ndiyo kigezo cha Mungu.” Loo, ni kweli jinsi gani. Akasema, “Lakini nitaenda mjini.” Naye akasema, “Hakuna mtu nchini, anayejua vizuri zaidi kuliko mimi, kwamba mimi si mhubiri mwenye nguvu.” Akasema, “Lakini Mungu aliniita kufanya kazi hii, nami ninajaribu kuifanya vizuri nijuaavyo, kwa ajili ya Mungu.” Ajabu; Mungu anaweza kumwinua mtu namna hiyo, naye abaki mnyenyekevu hivyo.

¹¹⁰ Lakini akasema, “Lakini ninaingia, na, tuseme, kulikuwa na waongofu *kadhaa*, waongofu elfu kumi katika mkutano huu wa majuma sita.” Kisha akasema, “Ninarudi baada ya mwaka mmoja au miwili, wala sipati mmoja kati ya kumi wa hao.”

¹¹¹ Loo, jinsi nilivyotamani ningesema tu jambo fulani. Lakini huyo mtu anatumia maisha yake kabisa kwa ajili ya Mungu. Yeye huwafikia watu, ambapo, kamwe hawangekuja kunisikiliza mimi.

¹¹² Lakini hii hapa sababu yake. Ninalipata katika mkutano wangu. Oral Roberts anawapata katika mkutano wake. Nasi tutawapata kila mahali. Lakini hapa ndipo lilipo: Wanashikwa tu na mhemko. Wala hawaongoki. Hawafanyiki mwaminio halisi, juu ya msingi wa Neno. Wanafanya tu maungamo baridi, ya kawaida, na huo ni kama ndio mwisho wake.

Basi mateso madogo ya kwanza yanayokuja na kusema, “John, ilikuwaje na sigara?”

“Naam, ahem.”

“Nilisikia ulikuwa kwenye mkutano wa Billy Graham.”

“Vema, mke wangu, siwezi kuvumilia zaidi. Nipatie John Ruskins yangu.” Mnaliona? Mnaona?

“Liddy, ilikuwaje kwa kile kipodozi? Ninaona unaachilia nywele zako zikue. Nilisikia ulikuwa kwenye mojawapo ya miamsho ya Branham.”

“Vema, mimi siwezi kuwa mwanachama wa kilabu hiki na kuishi kwa amani. Nitavirudisha tu vitu vyangu na kuupodoa uso wangu.”

¹¹³ Endelea, kuna mwanamke mmoja katika Biblia aliyepaka uso wake rangi akakutane na wanaume, naye Mungu akamlisha kwa mbwa. Hiyo ni kweli. Ikiwa unataka kuwa nyama ya mbwa kwa Mungu, endelea.

¹¹⁴ Lakini sasa hebu kidogo tu. Sikilizeni, nataka msikie jambo fulani. Ilikuwa? Hawakufika mbali vya kutosha. Wanaweza tu kuwa, walipata wazo jipya la Kristo. Lakini angalia, unapopata moyo mpya, roho mpya, na kisha Mungu anamweka Roho

Mtakatifu, Roho Wake moja kwa moja katika roho yako mpya, msalaba unafunikwa na manyoya. Haikwaruzi tena.

¹¹⁵ Wanaweza kusema juu yako chochote watakacho. Hakitakusumbua. Mbona, jamani, mizigo ambayo ulimwengu unakutupia, sababu yako kuonekana kuwa na nguvu sana katika Roho wakati hiyo roho mpya iko ndani yako, na Roho Mtakatifu akiyapiga-piga maisha yako moja kwa moja kuelekea Mbinguni na Neno la Mungu. Mbona, uko tu kama Samsoni. Utayanyanyua malango ya shaba ya Gaza, na kuyabeba hadi kwenye kilima fulani kiitwacho Kalvari, na kumwombea mtu huyo. Hakika. Msalaba una mbawa juu yake. Unasonga mbele tu kwa urahisi.

¹¹⁶ Na hiyo ndiyo sababu mpulizo mdogo tu huwapeperushia mbali. Hiyo ndiyo sababu tunachukua maelfu ya wanachama kwa mwaka kisha upepo unawapeperushia mbali. Mateso madogo ya kwanza, hawawezi kuyastahimili. Mahali pabichi pa kwanza panapokuja, panakwaruza, msalaba, kwa hiyo wanautupilia mbali. Hujaulainisha bado. Unaona? Mungu hukulainishia msalaba. “Jitwikeni nira Yangu, na mjifunze Kwangu. Nira Yangu ni laini.” Hakika ni laini.

¹¹⁷ Ikiwa utaundiwa tu kwenye utaratibu wa Mungu. Utaratibu Wake, sasa, si kusikiliza theolojia fulani au hotuba fulani ya kiakili, bali ni kupata ubatizo wa Roho Mtakatifu. Halafu unaanza, utaratibu unaanza kukusogeza, sio wewe kuusogeza na kusema, “Mbona hivi ndivyo ninavyofikiri unapaswa kuwa.”

¹¹⁸ Mungu alisema hivi ndivyo unavyopaswa kuwa. Kwa hiyo Roho Mtakatifu anatenda kazi moja kwa moja katika Neno. Nawe unaendelea tu moja kwa moja. Ni rahisi sana unapofanya hivyo. “Moyo mpya nitawapa.”

¹¹⁹ Sasa, nira laini. Mungu alitaka kuonyesha, kwa wanafunzi na kwa ulimwengu, uweza Wake. Hivyo wakati Kristo. . . Hebu tuangalie nguvu za Mungu zinazopaswa kuwa katika kanisa; ambapo kwa Roho mmoja sisi sote tunabatizwa kuwa Mwili mmoja. Na Mwili huo ni Mwili wa Kristo. Bila kujali dhehebu lako, ni Mwili wa Kristo kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mnaamini hilo? Ndiyo njia pekee unayoweza kuwa.

¹²⁰ Mungu anataka kuuonyesha ulimwengu ufufuo wa Kristo. Huyu hapo amelala kaburini. Yuko kimya; mwili Wake ni nweupe kama chaki. Na kwenye asubuhi ya Pasaka tunamsikia akisema kwa sauti kuu, “Mamlaka yote yamewekwa mkononi Mwangu! Karibuni nyote mkasikilize!” Nasi tunaona nguvu za uvutano zikipoteza nguvu zake, tunapooni mwanga ukija kati ya miguu Yake na nchi. Mbona? Yeye ndiye kitovu cha uvutano. Naye anainua juu, juu, juu. Ni nguvu za Mungu zikimwinua Yeye juu, kutuonyesha sisi, ya kwamba, kile ambacho Kanisa litafanya siku moja, kwa maana sisi, tukiwa tumekufa, tuko ndani ya Kristo, sehemu ya Mwili Wake na kama vile Mungu alivyomfufua

Kristo, Yeye ataliinua juu Kanisa Lake. Nawe unayo ndani yako sasa, hiyo nguvu mpya, iliyo hai. Loo, ni ajabu jinsi gani!

Nawataka muone, tena, jinsi ambavyo Mungu hulifanya. Yeye alisema, “Roho Yangu nitaiweka ndani ya roho yako, roho yako mpya.”

Nataka kuwaulizeni jambo fulani. Tunauwazia sana mwili huu wetu. Loo, jinsi ulivyo mkuu.

¹²¹ Si muda mrefu uliopita nilikuwa nimesimama huko Nashville, Tennessee, kwenye jumba la makumbusho. Nami nilikuwa nikitazama mambo mbalimbali. Napenda sanaa. Mungu yuko katika sanaa. Mungu yuko katika muziki. Nami nilikuwa nikiitazama sanaa hiyo, basi nikaona vijana wawili wamesimama pale, nayo ilikuwa inatoa uchanganuzi wa thamani ya mwili wa mtu wenye uzito wa pauni mia moja na hamsini. Unajua una thamani gani? Senti themanini na nne, hiyo ni kweli. Na kama nilivyosema asubuhi ya leo, utaweka kofia ya dola ishirini na tano kwenye senti themanini na nne, kuzilinda; koti la cheche la dola mia tano juu ya senti themanini na nne, ili kuzilinda. Hakika.

¹²² Loo, kama ungeona buibui katika supu yako, ungeulaani mkahawa huo na kukaa kwenye Baraza la Wafanyabiashara, na ungeliandika kwenye gazeti. Hakika, unazilinda hizo senti themanini na nne; lakini unamwacha ibilisi ashindilie chochote anachotaka ndani ya nafsi yako hiyo, iliyo na thamani ya dunia elfu kumi.

¹²³ Na wakati hawa vijana wawili wakisimama pale, wakitazama... Una takriban chokaa ya kutosha kunyunyizia kiota cha kuku, na vitu vichache, kalisi iliyo ndani yako, na kadhalika. Mmoja akamtazama mwenzake, akasema, “John, hatuna thamani kubwa sana sivyo?”

¹²⁴ Nilifikiri ningesimama, nikaweka mkono wangu juu yake. Nikasema, “Lakini kijana, unayo nafsi ndani yako ambayo ina thamani ya dunia elfu kumi, ambayo Yesu Kristo alikufa ili kuikomboa.” Hakika.

¹²⁵ Nilishangaa hapa wakati fulani kule Illinois, nikipitia sehemu ndogo, na kulikuwa na ju—jumba la makumbusho. Nilikuwa nikiangalia humo. Nikamwona mzee mweusi. Alikuwa na ukingo mdogo tu wa nywele. Alikuwa akipita mahali hapa, akitazama huku na huku. Mara akasimama; macho yake yakatazama tena, akaanza kulia. Alilia kwa dakika chache. Kisha nikamwona akiinamisha kichwa chake akaanza kuomba. Nikamtazama kwa muda kidogo, nikawazia, “Nini kimemshtusha huyu mzee? Vema, naamini nitatafuta kujua.”

Akatazama tena, na kufuta macho yake. Yeye ni mzee, mzee kweli. Nikasema, “U hali gani, mjomba?”

Akaangalia, akasema, “U hali gani?”

Nikasema, “Mimi ni mhudumu wa Injili, na ningependa kukuuliza swali. Nilikuona ukiomba. Kwa nini ulikuwa unaomba?”

Kasema, “Njoo hapa.” Nikaenda pale na kuangalia. Kasema, “Angalia pale.”

Nikasema, “Ni kitu gani kile? Ni vazi.”

¹²⁶ Akasema, “Lakini doa lile pale ni damu ya Abraham Lincoln.” Akasema, “Mzungu, bado kuna alama kiunoni mwangu ambapo mkanda wa utumwa ulikuwa wakati mmoja.” Akasema, “Damu hiyo iliniondolea ule mkanda wa utumwa. Si lingekusisimua?”

¹²⁷ Kama hiyo ingemsisimua mtu mweusi kwa kumwondolea mkanda wa utumwa, Damu ya Yesu Kristo inapaswa kumfanyia nini mwaminio? Unapoweza kupita chumba cha baa, ukumbi wa kucheza kamari, na mambo ya ulimwengu, na kujua uko huru, moyo wako ukidunda sawasawa na Neno la Mungu, ukijua ya kwamba siku moja unaenda Nyumbani. Hilo si lingemsisimua mtu yeyote? Ni jambo la kulisimua.

¹²⁸ Mimi huwa nashangaa wakati mwingine . . . ninapopitia nchi ya kusini. Nilisikia hadithi ambayo nilisimuliwa. Katika zile siku walipokuwa wakinunua watumwa hao, kulikuweco na mnunuzi ambaye angetoka na kuwanunua hao wanaume, kama vile tu unavyonunua gari la mtumba siku hizi; wanadamu. Naye angenunua kundi moja hapa, na kununua kundi kule. Kwa hiyo akapitia kwenye shamba kubwa lenye watumwa wengi. Naye alitaka kununua kadhaa.

¹²⁹ Ndipo akaona kulikuwa na kijana mwanamume mmoja pale aliyekuwa tofauti na wanaume wengine. Sasa, walikuwa mbali na nyumbani. Niliwahubiria huko Afrika. Nami najua tabia zao na kadhalika. Basi wakati wao . . . Wa—Waholanzi walikwenda kule, na kuwachukua, na kuwaleta huku, na kuwauza kama watumwa. Nao walikuwa mbali na nyumbani; walivunjika moyo. Walikuwa na vitu vingi, na nyumbani, na wapendwa wao. Hawangerudi nyumbani tena. Walikuwa mtumwa. Walikuwa nje ya nchi yao. Nao ha—hawakuwa na ujasiri wa kufanya kazi wala chochote kile, na wangechukua mijeledi na kuwacharaza. Nao wangepaza sauti, “Endeleeni kuvuta.”

¹³⁰ Basi siku moja, mnunuzi huyu akamwona kijana mwanamume mzuri ametanua kifua chake, kichwa chake juu. Haikukubidi kumcharaza. Alikuwa macho. Kila wakati jambo lolote lilipotakiwa kufanywa, alilifanya. [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.]

Ndipo mnunuzi huyu wa watumwa akasema, “Nataka kumnunua.”

Naye mwenyewe akasema, “Hauzwi.”

Akasea, “Ni kitu gani kinachomfanya mchangamfu hivi?”
Kasea, “Je, yeye ni bosi juu ya hao wengine?”

Kasea, “La, yeye ni mtumwa tu.”

Kasea, “Je, unamlisha vizuri zaidi kuliko hao wengine?”

Kasea, “Hapana, anakula kwenye manchani pamoja na hao wengine.”

¹³¹ “Basi ni kitu gani kinachomfanya awe tofauti sana na mchangamfu? Ari yake inaonekana kuwa juu sana, ari yake.”
Kasea, “Ni kitu gani kinachomfanya tofauti sana na hao wengine?”

¹³² Akasea, “Mimi mwenyewe sikujua, mpaka nilipogundua hivi majuzi kuwa baba yake ni mfalme wa hilo kabila. Na ingawa yeye ni mgeni katika nchi nyingine, anajua baba yake ni mfalme. Naye anatenda na kuenenda kama mwana wa mfalme.”

¹³³ Mkristo anapaswa kufanya nini basi? Sisi ni wasafiri na wageni, lakini Baba yetu ni Mfalme. Je, tunapaswa kutenda na kuishi vipi katika ulimwengu huu wa sasa? Sio kama ulimwengu huu, si kusukumwa huku na huku, na kutia sahihi tiketi tutakuja kanisani, na—nasi tutajaribu tuwezavyo kufanya hivi, nasi tutaenda kwenye mkutano unaofuata wa maombi.

¹³⁴ Ndugu, dada, tunapaswa kuenenda kama wana na binti za Mungu. Hatupaswi kurudi nyuma wakati shetani anapojaribu kulichafua Neno la Mungu. Hilo ni Neno la Baba yetu. Hebu na tulitetea Hilo mpaka tufe. Naam, bwana. Jiadabishe.

¹³⁵ Ingawa tuko katika nchi nyingine, labda katika nchi nyingine, unaweza kuwa katika nchi nyingine ambayo iko mbali sana, m—mgeni. Lakini haileti tofauti yoyote jinsi ulivyo mbali, ni shida gani ulizo nazo, Mungu angali ni Baba yako. Haleluya! Ulitoka wapi?

¹³⁶ Huko nyuma kabisa hapo mwanzo wakati Mungu alipomtuma Logos, ambaye alikuwa ni Mwana wa Mungu kutoka katika kifua cha Baba, alianza kuatamia juu ya dunia, Biblia ilisema.

¹³⁷ Neno *kuatamia* ni nini? Lina maana gani? Kama “malezi,” kama kuku, makinda yake huitwa vifaranga wake, watoto wake. Naye Roho Mtakatifu, tuseme, kwa mikono Yake, ama, mbawa Zake zikiatamia nchi ya ukiwa, ambapo hapajapata kuwa na uhai. Naye alipoanza kuatamia, maji yakaanza kutengana, nayo nchi ikatokeza. Mwili wako ulikuwa umelala hapa duniani wakati huo. Umeumbwa kutokana na elementi kumi na sita za dunia hii. Mwili wako ulikuwa hapa wakati huo. Angalia, kama haukuwako, ulitoka wapi? Unaishi kwa vitu vilivyokufa.

¹³⁸ Unapokula nyama ya ng’ombe, ng’ombe alikufa. Ukila mkate, ngano ilikufa. Unaweza kuishi tu kwa vitu vilivyokufa. Sasa, nilimuuliza daktari hivi majuzi, nikasema, “Daktari, ni kweli kwamba ninapokula, ninafanya upya maisha yangu?”

Akasema, “Hiyo ni kweli.”

¹³⁹ Nikasema, “Basi, Daktari, ni kwa nini nilipokuwa na umri wa miaka kumi na sita, nilikula chakula kile kile ninachokula sasa, nilikuwa nikizidi kuwa mkubwa na mwenye nguvu zaidi, huku maisha yangu yakifanywa upya, nami ninakula chakula kile kile sasa, na ninazidi kuzeeka na kudhoofika na kupungua? Nithibitishie kisayansi, juu ya, *hiki* hapa chombo na hii *hapa* jagi ya maji, nawe unamiminia maji ndani yake, nayo inajaa kufikia mahali fulani, halafu, kadiri unavyozidi kuyamimina mle, ndivyo yanavyozidi kupungua. Kuna jibu moja tu: Mungu amepanga.” Kifo huingia unapokuwa na umri wa kati ya miaka ishirini na miwili hadi ishirini na mitano, mvi huanza kutokea, makunyanzi usoni. Nawe unakula chakula kile kile, ukifanya upya maisha yako, lakini unakufa. Mungu amepanga.

¹⁴⁰ Sikilizeni sasa, katika kumalizia, ningetaka kusema hili sasa kwa usikivu wenu mkamilifu. Loo, laiti mngaliweza kulishika. Angalia, huyo hapo wewe umelala duniani hapo mwanzo. Naye daktari huyu niliyekuwa nikizungumza naye alikuwa kafiri. Alikuwa akidhihaki uponyaji wa Kiungu. Ndipo nikasema, “Daktari, nataka kukuuliza jambo fulani.”

“Loo, kuzaliwa kwako na bikira na upuuzi huo wote,” akasema.

Nikasema, “Daktari, hebu kidogo. Kama inabidi kitu fulani kife ili mwili wangu upatikanao na mauti uishi, Daktari, je, kuna kitu cha kiroho ndani yangu?”

“Naam.”

¹⁴¹ “Lazima kuwe na nafsi mle ndani inayonipa maarifa ya kujua mema na mabaya na kadhalika. Basi kama ilibidi kitu fulani kufa ili mwili huu uweze kuishi, kwa hiyo, ilibidi Kitu fulani kife ili nafsi yangu iweze kuishi.” Nami nikamwangalia. Akaniangalia tena, akatikisa kichwa chake, akaondoka.

¹⁴² Ndipo Roho Mtakatifu alipoanza kuatamia juu ya nchi, angalieni, hebu na tuvute taswira kidogo. Ni ukiwa; ni tupu. Angalieni kilichotokea. Alipoanza kuatamia, ninaweza kuona unyevu kidogo ukitokea, na kuzunguka hapo zikajifungia baadhi ya vitamini na elementi zinazolingia katika ua. Ndipo ua dogo la Pasaka likatokea. Nini kilisababisha hilo? Ati maarifa? La, kuatamia kwa Roho Mtakatifu.

¹⁴³ Kisha nyasi zikatokea; mimea ikatokea. Roho Mtakatifu akaendelea kuatamia. Baba akasema, “Hilo ni zuri sana.” Kisha ikatokea miti ya matunda. Halafu kutoka huko ndege wakaruka kutoka mavumbini. Roho Mtakatifu akaendelea kuatamia, akinong’oneza, akifanya mapenzi, akiatamia kutoka duniani. Kutoka huko ukaja uhai wa wanyama. Kisha baada ya muda kidogo akaja mtu. Roho Mtakatifu akiatamia kutoka katika nchi, akiatamia juu ya nchi, akamleta pamoja mtu, kutoka hapo, zaotuka, Yeye alimfanya mwanamke.

Na hao wapenzi, walipokuwa wakitembea katika bustani ya Edeni pamoja, ninaweza kumsikia Hawa akisema, “Loo, upepo ni mbaya sana.”

¹⁴⁴ Namsikia mume akisema, “Amani, tulia.” Na upepo ukatulia. Pia ninaweza kumsikia akisema, “Mpenzi...” huku mke akiweka maskini kichwa chake juu ya mabega yake, huku wakizunguka-zunguka, wasiwe wagonjwa kamwe. Hakuhitaji kuwa na Vipodozi vyovyote ili kujifanya aonekane mrembo. Alikuwa awe hivyo milele. Na huku mikono yake ikiwa imeukumbatia mkono mkubwa wa Adamu, walitembea kama wapenzi kwenye hiyo bustani. Na baada ya kitambo kidogo, Leo, yule simba, akanguruma. Hakukuwa na hofu yoyote. Akasema, “Njoo hapa, Leo.” Naye akampapasa mgongoni. Duma, simbamarara akaja hapo; akampapasa. Nao wakawafuata nyuma yao kama paka wadogo.

¹⁴⁵ Ndipo jua likaanza kutua siku ya kwanza, ama, siku ya sita, hasa. Basi lilipoanza kutua, Adamu anasema, “Mpenzi, hatuna budi kwenda kanisani usiku wa leo. Lazima twende kwenye kanisa kuu.” Basi walipoiendea ile miti mikubwa na kupiga magoti, yule Logos mwororo anayemeka, Mungu, akashuka chini kupitia humo mitini.

¹⁴⁶ Nasikia Sauti Yake ya upole ya Baba ikisema, “Watoto, mmefurahia kukaa duniani leo?” Naye anawabusu shavuni, tuseme, na kuwalaza kitandani. Simba, akamlaza chini, na Duma yule simbamarara; hakuna madhara, hamla hatari.

¹⁴⁷ Je, hungependa kufanya hivyo tena? Lakini je, inawezekana? Naam, bila shaka. Na kama Roho Mtakatifu akiuatamia mwili wako kutoka ardhini, bila wewe kuwa na fununu ya kile utakachokuwa, au ujuzi wowote wa kuja kwako, na angeweza kukuleta hadi hapo ulipo, na kukupa chaguo, ni zaidi sana vipi itamchukua Roho Mtakatifu kukuatamisha kutoka ardhini, haijalishi kama mwili wako umetawanyika kwenye pepo nne za dunia?

¹⁴⁸ Wewe uliletwa na kitu gani, kwanza kabisa? Wewe ni mavumbi; dhambi iliingia ndani, nasi hatuna budi kwenda, bado tungali... Mungu kamwe hatashindwa. Alitarajia dunia hii ikaliwe, kwa hiyo akawafanya tu wanawake wapate kuzaa watoto. Angali anamwaga kalisi, na potashi, na e—elementi ndani yao, na kuwaimarisha. Kisha anawafikisha mahali na kukuacha ujichagulie.

¹⁴⁹ Na ikiwa, bila kujichagulia, Mungu alinifanya siku moja kuwa kijana mwanamume, mwenye nguvu, mwenye afya njema, na mwenye furaha, naye Roho Mtakatifu (Si baadhi ya mafundisho ya sharti ya the—theolojia baridi, yenye taratibu, ya seminari, lakini Roho Mtakatifu mbarikiwa; si mti wa maarifa, bali Roho Mtakatifu, mnaona, ni mpango wa Mungu.) akaanza kuniatamia na kunifanyia mapenzi, nami nikamkubali, kisha

akashuka moyoni mwangu na kuchukua mahali Pake, je, ni zaidi sana vipi nina uhakika kwamba atanifufua katika siku za mwisho?

¹⁵⁰ Mbona, Yeye aliahidi, a—aliapa kwake. Na uthibitisho wake moyoni mwangu sasa hivi, na moyoni mwako, ya kwamba atatufufua katika siku za mwisho. Kwa hivyo uzee au kitu kingine chochote kinajalisha nini? Si kitu. Mungu alitoa ahadi. Roho Mtakatifu analitawala kanisa. Roho Mtakatifu alikuleta hapa. Kitu hicho chote kimefungwa ndani ya Roho Mtakatifu.

Sasa, Roho Mtakatifu anapokunong'onezea, na kusema, “Mwenye dhambi, wewe ni zawadi ya upendo wa Mungu, nataka kukufanya mapenzi,” hivi hutakubali?

¹⁵¹ Kwa nini usiufungue tu moyo wako na kusema, “Naam, Roho Mtakatifu, mimi hapa. Mimi hapa. Loo, sijali mtu yeyote anasema nini. Roho Mtakatifu, ninakutaka Wewe. Ninakutaka Wewe. Wewe Ndiwe ninayemtafuta. Wewe Ndiwe”?

¹⁵² Ndipo pepo mchafu akimtoka mtu, ibilisi, kisha anarudi kwenye kichochoro chake cha kale cha mkebe wa bati kilichokuwa kikikufanya unywe pombe, na kupiga makelele, na kukoroma, na kushuku, na kuzozana, na kubishana kuhusu Biblia, anaporudi kwenye kichochoro chake cha kale tena, unajua nini kinachotukia? Mungu alituma buldoza Yake kubwa kutoka Mbinguni akakisafisha hicho kichochoro cha kale. Naam, bwana, kile kibanda cha kale kimekwisha; ile mkebe ya bati imekwisha; takataka zimekwisha. Yote yamesukumizwa kwenye Bahari ya Usahaulifu, Naye akayasawazisha.

¹⁵³ Naye akajenga nyumba kubwa, ya kisasa. Naye amekuwa akiatamia kule, na yungiyungi nzuri zimechipuka uani kote hapa. Nyasi za kupendeza zinamea, na barabara kuu mno inapitia mle. Ati nini? Kumekuwa na mtu mpya aliyehamia mle, si yule mzee ambaye wakati mmoja alikaa hapo, ambaye alikufanya ugombane, ulaani, umtendee jirani yako vibaya, uwe mfuasi wa dhehebu, mwenye mawazo finyu, mwenye kushuku, wa kikafiri, pamoja na maskini dini iliyoanguliwa kukufanya uchefuke. Bali amekusafisha, Roho Mtakatifu pale na kuatamia. Wakati Roho Mtakatifu akiatamia, ataleta upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, upole, uvumilivu. Atapamba nyumba Yake sawasawa. Hakika, Yeye atakuondolea kichochoro hicho cha kale cha mkebe wa bati . . . hapo, kinachosababisha mashaka na mizozo yenu ya kale na kadhalika. Ataweka njia kuu kupita humo, ili mambo yote yaende sawa kwako. Amina.

¹⁵⁴ Ee, ndugu, tunachohitaji leo hii si meya mpya wa jiji, sio polisi wapya kwenye kikosi, si dhehebu jipya, si ukarabati wa kanisa, bali tunahitaji uamsho wa Mtakatifu Paulo wa mtindo wa kale na Roho Mtakatifu wa Biblia kurudi kanisani tena: Wamethodisti, Wabaptisti, Wapentekoste, na ninyi nyote. Ni

kweli hasa. Tunachohitaji leo, mtu aliye na ujuzi huu wa kuwa mpinzani, mtu anayemjua Mungu ajitokeze.

¹⁵⁵ Hapa si muda mrefu uliopita nilipokuwa Uswisi... Sikilizeni kwa makini, tunapofunga. Ni wangapi, na zaidi sana ninyi wanaume wa rika yangu, wanawake, mmesoma hadithi maarufu ya Arnold von Winkelried? Wengi wenu mnamkumbuka, yule shujaa mkuu wa Uswisi. Loo, hadithi hizo zinasahaulika kwa urahisi sana miongoni mwa watu. Ushujaa wake haujawahi kupitwa na umelinganishwa kwa nadra sana.

¹⁵⁶ Siku moja wakati Waswisi walipotoka na kupata nyumba zao ndogo na kadhalika katika milima ya Uswisi, na Wakristo wanaoomba, basi walipokuwa na nyumba zao ndogo na kila kitu cha kupendeza, jeshi kubwa la wavamizi liliingia. Waswisi wakakusanyika chini ya milima na majembe makuukuu, au kulabu, ndoano za kupogoa na chochote ambacho wangeweza kuwa nacho cha kupigana. Hawakuwa watu wa vita. Walikusanyika tu wakiwa na fimbo, na mawe, na chochote ambacho wangeweza kupigania kuilinda nchi yao.

¹⁵⁷ Lakini watoto wao wachanga na mama zao, ambapo hao askari walikuwa wameingia na kuwaua watoto wao wachanga, na kuwabaka wanawake mitaani, na chochote kile, na kuzibomoa nyumba zao na kuchukua riziki zao. Basi hili hapa jeshi kubwa linakuja, lililo na silaha kamili, lililofunzwa vizuri: pum, pum, pum, mikuki mirefu, wamefunzwa vizuri, kama ukuta wa matofali, wanakuja wakiingia maskini Uswisi.

¹⁵⁸ Loo, ilionekana giza sana. Basi maskini jeshi dogo la Uswisi, lililosukumiwa pembeni mwa mlima, lilishindwa kabisa. Walitazama huku na huku, na ninii tu, loo, wamezidiwa kwa maelfu. Na zana walizokuwa nazo za kupigana, silaha zao, hazikuwa kitu cha kulinganishwa na mikuki hiyo mikubwa mirefu. Ulinzi wao haukuwa kitu, vifua vyao vitupu vikawa tu shabaha ya hiyo mikuki waliyorushiwa, wakati hao wengine walikuwa wamefunikwa vizuri na ngao.

¹⁵⁹ Hawakufundishwa; walikuwa bila mafunzo, wakati jeshi hilo lingine lilikuwa limefunzwa, na kila hatua vivyo hivyo. Likazidi kusonga mbele zaidi na zaidi. Hatimaye, jambo fulani halina budi kutendeka. Uchumi wao mdogo wa taifa la Uswisi ulikuwa hatarini; kila kitu kilikuwa hatarini.

¹⁶⁰ Hatimaye, kijana mmoja jina lake Arnold von Winkelried akajitokeza, naye akasema, "Wanaume wa Uswisi, siku hii nitatoa maisha yangu kwa ajili ya Uswisi." Kasema, "Kitu fulani lazima kifanyike, nami nitakifanya." Akasema, "Ng'ambo ya mlima huu kuna nyumba ndogo nyeupe, ambamo maskini mke mzuri, mpendwa, na watoto watatu wadogo wanakungojea kurudi kwangu; lakini hawataniona tena, kwa kuwa leo hii nitautoa uhai wangu kwa ajili ya Uswisi."

Ndipo watu wote wakashangaa, wakasema, “Arnold von Winkelried, utafanyia nini Uswisi?”

Akasema, “Nifuateni tu. Nifuateni, na mpigane na mlichio nacho, vizuri mwezavyo.”

¹⁶¹ Ndipo akatupa chini alichokuwa nacho. Naye akatupa mikono yake juu kuelekea angani, na kupiga kelele kwa sauti yake yote, na kusema, “Fungueni njia uhuru upite! Fungueni njia uhuru upite!” Naye alipokuwa akikimbia kuelekea kwenye jeshi la Uswisi, alitazama aone mahali mikuki iliposongamana sana, akajitosa mahali hapo akiwa ameinua mikono juu. Ndipo mikuki mikali mia moja ikajielekeza kumnyanyua juu. Basi alipofika hapo alinyakua lundo zima la hiyo, akaichomelea kifua ni mwake, akaanguka akafa. Ni, onyesho kama hilo la ushujaa lililishinda kabisa jeshi hilo. Hawakujua la kufanya; ni sawasawa na Daudi na Goliathi.

¹⁶² Nao hao askari wa Uswisi wakaona kilichotukia, nao wakaingia mbio, na majembe yao, na miundu yao, na mawe yao, walilifukuza jeshi hilo nje kabisa ya hilo taifa. Na wamekuwa na amani tangu wakati huo. Hakujawa na vita nchini Uswisi. Taja tu Arnold von Winkelried milimani na utazame mashavu yakibadilika rangi na machozi yakitiririka. Wanajua kile nchi yao ya amani, ilichogharimu; onyesho kubwa jinsi hiyo la ushujaa.

¹⁶³ Lakini loo, hilo lilikuwa jambo dogo sana, kulinganisha, na jambo lililotukia siku moja.

¹⁶⁴ Wakati jamiini ya Adamu, watoto wa Adamu, wote walikuwa wamesukumiwa pembeni, mauti na magonjwa kila upande, dhambi ikilundikana ndani; sheria ilikuwa imeshindwa; manabii walikuwa wameshindwa; kila kitu kilikuwa kimeshindwa; walikuwa wamekataa, nao walikuwa katika mchafuko mkubwa. Magonjwa na ujinga, na kadhalika, yalikuwa yamewaporomoshea tu mahali fulani mpaka hapakuwapo na matumaini yaliyosalia. Na hapo ilisimama jamii ya Adamu ikitikisika, ikitetemeka. Hakuna kitu kingeweza kufanywa; kuzimu ilikuwa inafungua kifua chake kuwameza. Na katika Utukufu, Mtu fulani alitokea, Mwana wa Mungu: “Nitashuka, Baba. Nitakuwa mmoja wao. Nitashuka.”

“Utafanya nini?” walisema Malaika.

“Angalieni.”

¹⁶⁵ Siku moja, akisimama kule miongoni mwa wana wa binadamu, alitazama chini kupitia ile hofu kuu sana aliyokuwa nayo mwanadamu, ambayo ilikuwa ni kifo, na alipoinua mikono Yake na kwenda mahali paitwapo Kalvari, alijitumbukiza Mwenyewe katika ukungu wenye giza kuu sana ambao mwanadamu aliwahi kuogopa, ambao ulikuwa ni mauti, akaushinda. Ndipo alipopaa Juu, hakushusha azimio la imani ya kitheolojia; alimrudisha Roho Mtakatifu, akasema, “Mchukue

Huyu, na upigane na kila kitu ulicho nacho ndani yako. Mchukue Huyu, na unifuuate. Kama vile Baba alivyonituma Mimi, nami nawatuma ninyi.” Naye Baba aliyemtuma, alienda pamoja Naye, na kuingia ndani Yake. Naye alipotutuma, alikuja pamoja nasi, ndani yetu.

¹⁶⁶ Enyi wanaume na wanawake, tunachohitaji leo hii sio majina yetu kwenye kitabu cha kanisa, ambalo ni sawa kabisa, lakini tunahitaji kuchukua hiyo Silaha yenye nguvu ya Roho Mtakatifu ndani ya mioyo yetu, ambayo hubadilisha utu wetu wa ndani kabisa, na kutufanya kuwa viumbe vipya katika Kristo Yesu, na kufanya njia katika ulimwengu wa dhambi kwa haki na nguvu za ufufuo wa Yesu Kristo.

¹⁶⁷ Hilo ndilo tunalohitaji. Hilo ndilo kanisa linalohitaji, sio ukarabati au kundi la washiriki wapya, bali ni kufufua yale tuliyo nayo, na kujazwa na Roho Mtakatifu, na kwenda kupigana na adui, kuwaombea wagonjwa, kuwaponya wagonjwa, kuwatoa pepo. “Mnapokea bure, toeni bure. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Kristo aliweka mkononi mwa mwanadamu silaha yenye nguvu kuliko zote ambazo zimewahi kuwekwa kwa wanadamu, ilikuwa ni ubatizo wa Roho Mtakatifu: moyo mpya, roho mpya, “nami nitaweka Roho Yangu mle ndani.” Na basi mpigane na yaliyomo ndani yenu mpaka kifo kitakapowaweka huru.

Na tuombe.

¹⁶⁸ Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, kabla hatujasonga mbele zaidi, najiuliza hivi: enyi wanaume na wanawake, je, mnajua ya kwamba kuna Kitu kimoja tu kinachoweza kuwapa Uzima, na hicho ni Roho Mtakatifu? Je, mnatambua kuwa Yeye Ndiye anayeatamia juu yenu?

¹⁶⁹ Wakati mtoto huyo mchanga alipochukuliwa, nawe ukampeleka kaburini, ukapigapiga maskini mashavu yake madogo, na kusema, “Mpenzi, mama atakutana nawe, baba atakutana nawe.” Ilikuwa ni nini? Ilikuwa ni Roho Mtakatifu akiatamia.

¹⁷⁰ Wakati siku baada ya siku, unapopiga magoti ili kuomba sala hiyo ndogo kabla ya kulala, na Kitu fulani kinakwambia kuna kitu kimeenda kombo kabisa, Yeye ni mvumilivu, hapendi yeyote aangamie. Je, unatambua kwamba huko ni kuatamia kwa Roho Mtakatifu?

¹⁷¹ Je, unasema, “Mwaka ujao nitajaribu kufanya vizuri zaidi; wakati mwingine watakapokuwa na uamsho nitaenda madhabahuni; labda nikipata nafasi na kazi yangu imekamilika, nitapata muda kidogo wa kuomba”? Loo, unafanya hivyo? Roho Mtakatifu anaatamia. Sikujui wewe; Mungu anakujua.

¹⁷² Lakini nataka wewe umwinulie Kristo mikono yako sasa hivi na kusema, kwa kuinua mikono yako, “Ee Kristo, sasa najua ya kwamba Roho Wako Mtakatifu amekuwa akiatamia juu

yangu kuniita nikutumikie Wewe.” Loo, huenda usiwe mhubiri au mmishenari. Huenda ukawa tu ni mfuasi wa kanisa katika kanisa lako. Lakini Roho Mtakatifu anakuita. Anataka uwe na ushuhuda kwa ajili ya kanisa hilo. Je, unaweza kumwinulia mkono wako sasa hivi, kama ishara ya kusema, “Mungu, ni mimi; ninajibu sasa”?

Mungu akubariki. Loo, jamani. Juu kwenye roshani, juu waliomo mle ndani. Mungu awabariki huko nyuma. Loo, hilo ni jema.

¹⁷³ Ee Baba wa Mbinguni, mkutano mmoja zaidi, kisha huu uamsho mdogo utafungwa, kadiri tunavyojua. Na tunaposimama, usiku baada ya usiku, na kumwona Roho Mtakatifu akiatamia, akiondoa mateso kutoka kwa watu, akifunua siri za mioyo yao, akionyesha matendo makuu yenye nguvu, na ishara, tunatambua tuko mwisho wa safari.

¹⁷⁴ Ulisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu...” Ulimwengu ulikuwa umekuwa wa kimitambo, ujenzi wa nyumba, chuma, metali, kadhalika, halafu, kwa ghafla, kutoka katika ulimwengu huo baridi, wenye utaratibu, wa kidini, akainuka nabii, Malaika akatokea, ishara zikaanza kutukia, ndipo ulimwengu ukaangamizwa.

¹⁷⁵ Wakitoka Misri mamia ya miaka baadaye, wakati kanisa lilikuwa limepoa na sherehe zao za kidini zilikuwa baridi sana na zenye taratibu na za kutojali, ilikuwa tu ni karibu wakati wa kwenda nyumbani: Malaika akatokea; nabii akazaliwa; ujumbe ukatolewa; ishara na maajabu yalifanyika; miujiza ikatokea, mambo ambayo yalikuwa yamekufa kwa miaka mingi, nao walikuwa wakiyakana; ilikuwa ni mwisho wa safari.

¹⁷⁶ Basi walipoingia baridi tena, kabla tu ya Kuja kwa Bwana Yesu: Malaika akatokea; nabii akazaliwa; ya kimbinguni yakafanyika; ndipo Mwana wa Mungu akaja ulimwenguni.

¹⁷⁷ Na Baba, limepoa sasa kwa miaka hii yote. Na sisi hapa kwenye njia panda tena: ulimwengu baridi, wenye taratibu pamoja na jaketi zao za kikanisa, desturi za kidini, kujiunga kwao na kanisa, nao wanakuwa tu wagumu, wanaweza kuona kwa macho yao wenyewe kwamba ya kimbinguni yanafanywa; Malaika wanaonekana; ujumbe umeenezwa; kazi za Mungu zinadhihirishwa. Ee Mungu, utikise kila moyo.

¹⁷⁸ Na katika jengo hili dogo, alasiri ya leo, ambapo ni wachache wetu tu tumekusanyika pamoja, kumekuwako na madazeni ya mikono ambayo imeinuliwa. Wanataka Gurudumu hili katikati ya gurudumu. Wanataka Roho Wako katika maisha yao awatawale, na kuwafanya viumbe vipya, na kuwatawala, na ku—kuwapa maisha ya Kikristo na kuishi ndani yao.

¹⁷⁹ Nami ninaomba, Baba wa Mbinguni, kwa moyo wangu wote, ya kwamba utatuma ubatizo wa Roho Mtakatifu sasa hivi. Jalia utoke Utukufuni kama upepo wa kasi na kutua kwenye

kila moyo. Na jalia roho ya kale ya mbwa mwitu iwaache na ujalie Roho mpole na mtulivu wa Mwana-Kondoo aje, na Hua wa amani atatua juu ya Mwana-Kondoo kama alivyofanya huko Yordani siku ile. Kwa maana hao ndio viumbe wawili pekee wanaoweza kuendana pamoja. Nasi tunatambua, roho ya kale ya mapigano, katili, ya ulimwengu: Roho Mtakatifu asingeweza kukaa mahali kama hapo. Yeye hu—huruka tu akaenda Zake. Nasi tunajua hilo lingekuwa ni jambo lile lile, kama Mwana-Kondoo huyo angelithubutu kutenda kama mbwa-mwitu. Lakini ilibidi awe ni Mwana-Kondoo.

¹⁸⁰ Ee Mungu, leo hii, katika Utu Wako Mwenyewe wa uumbaji, jalia Roho Mtakatifu aatamie, sasa hivi, kwa mikono hiyo iliyoinuliwa juu na mingine mbali na hiyo, watabadilisha asili yao kuwa mwana-kondoo, roho mpya, moyo mpya; na jalia Hua aje akakae juu ya mioyo yao, awaongoze, na awape Uzima wa milele. Baraka hii ninaomba, kwa ajili ya kanisa hili dogo na watu hawa, katika Jina la Mwanao mpendwa, Bwana Yesu. Amina.

¹⁸¹ Mnampenda? Unajisikia tu kama umesuguliwa kabisa? Niliwaweka kwa muda mrefu kidogo. Saa kumi na nusu; nami nadhani watakuwa wakizisambaza kadi za maombi yapata saa kumi na mbili u nusu, kitu kama hicho, saa kumi na mbili ama saa kumi na mbili na nusu.

¹⁸² Sasa, ninawatakeni mfanye jambo hili, ninyi mlioinua mikono yenu na ninyi ambao mlipaswa kuinua. Siwaambieni mbadilishe makanisa yenu. Hapana, bwana, hapana. Wewe nenda tu kwa Kristo na umwishie kwa moyo wako wote.

¹⁸³ Nenda, ukamwambie mchungaji wako, wakati Roho Mtakatifu amekujaza, na useme tu, “Mchungaji, nitakuwa mfuasi tofauti na vile nimekuwa. Maisha yangu yatakuwa tajiri na ya kifalme, kwa sababu ndani yangu anakaa Roho Mtakatifu.” Loo, jinsi atakavyothamini hilo. Na labda unaweza kumwongoza kwenye tukio lilo hilo, ikiwa hajawa nalo tayari. Nani ajuaye? Hayo ndiyo tunayotaka.

Bwana awabariki. Nanyi ni kusanyiko zuri la kuzungumzia. Nami ninaomba ya kwamba kila mmoja wenu atajazwa na Roho Mtakatifu wa Mungu.

Ni wangapi wanaoamini niliyosema ni kweli, ya kwamba hiyo ndiyo haja ya kanisa? Asanteni. Na Bwana awabariki.

¹⁸⁴ Sasa, nitamwomba mchungaji, Ndugu Vayle, kama atakuja hapa na kuimalizia ibada, ninapoenda kuomba na kujiandaa kwa ajili ya ibada ya uponyaji usiku wa leo. Mungu akubariki, Dk. Vayle.

[Ndugu Vayle anazungumza na Ndugu Branham—Mh.]
(Naam, nadhani, kabla ya ibada za uponyaji. Nadhani.)

¹⁸⁵ Ndugu Vayle alikuwa akiuliza, walitaka picha fulani. Picha hizo zinaweza kupigwa wakati wowote, ninii tu, mpaka uvuvio utakapotokea kwa ajili ya ono, maana ile Nuru ninayoitazama, Hiyo—Hiyo ni Nuru.

¹⁸⁶ Ni wangapi wanajua ya kwamba Yesu Kristo ni Nuru sasa? Bila shaka, mtu yeyote anayeijua Biblia, anajua hilo. Bila shaka. Alikuwa ndiye . . . Wakati wowote ninapohubiri ama kadhalika usiku wa leo, itakuwa sawa kabisa. Bwana awabariki kwa wema wote wa Mbinguni, ndilo ombi langu. 

57-0127A Ugaji Wa Ukristo
Memorial Hall
Lima, Ohio Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org